**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Kamal Basha Pandu | Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo. |
| 2.Mhe. Ali Mzee Ali | Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais. |
| 3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe. |
| 4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge. |
| 5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni. |
| 6.Mhe. Haji Omar Kheri | Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu. |
| 7.Mhe. Haji Faki Shaali | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni. |
| 8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani. |
| 9.Mhe. Hamza Hassan Juma | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura. |

| | |
|---|---|
| 10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais. |
| 11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe. |
| 12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki | MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais. |
| 13. Mhe. Machano Othman Said | Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni. |
| 14.Mhe. Samia Suluhu Hassan | MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake. |
| 15.Mhe. Burhan Saadat Haji | MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni. |
| 16.Mhe. Asha Abdalla Juma | MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais. |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi. |
| 18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry | MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais. |
| 19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki. |
| 20.Mhe. Zainab Omar Moh'd | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake. |
| 21.Mhe. Idi Pandu Hassan | Mwanasheria Mkuu wa Serikali. |

| | |
|---|---|
| 22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae. |
| 23. Mhe. Mzee Ali Ussi | Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani. |
| 24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari | Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu. |
| 25.Mhe. Khamis Jabir Makame | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni. |
| 26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole. |
| 27.Mhe. Tafana Kassim Mzee | Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini. |
| 28.Mhe. Zahra Ali Hamad | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake. |
| 29.Mhe. Zakiya Omar Juma | "Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake. |
| 30.Mhe. Said Ali Mbarouk | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando. |
| 31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga. |
| 32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake. |

| | |
|---|---|
| 33.Mhe. Hamad Masoud Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole. |
| 34.Mhe. Omar Ali Shehe | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake. |
| 35.Mhe. Rashid Seif Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani. |
| 36.Mhe. Mohamed Ali Salim | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani. |
| 37.Mhe. Asaa Othman Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete. |
| 38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake. |
| 39.Mhe. Najma Khalfan Juma | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake. |
| 40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile. |
| 41. Mhe. Abass Juma Muhunzi | Jimbo la Chambani. |
| 42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. |
| 43.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini. |
| 44.Mhe. Ali Denge Makame | Jimbo la Amani. |
| 45.Mhe. Ali Haji Ali | Jimbo la Mkwajuni. |

| | |
|---|---|
| 46.Mhe. Ali Moh'd Bakari | Jimbo la Tumbe. |
| 47.Mhe. Ali Suleiman Ali | Jimbo la Kwahani. |
| 48.Mhe. Ame Mati Wadi | Jimbo la Matemwe. |
| 49.Mhe. Ame Ussi Juma | Jimbo la Nungwi. |
| 50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake. |
| 51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila | Jimbo la Fuoni. |
| 52. Mhe. Asha Moh'd Hilal | Jimbo la Magogoni. |
| 53.Mhe. Ashura Abeid Faraji | Nafasi za Wanawake. |
| 54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Nafasi za Wanawake. |
| 55.Mhe. Dadi Faki Dadi | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba. |
| 56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim | Nafasi za Wanawake. |
| 57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | Jimbo la Mji Mkongwe. |
| 58.Mhe. Haji Mkema Haji | Jimbo la Koani. |
| 59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji | Uteuzi wa Rais. |
| 60.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani. |
| 61. Mhe. Juma Duni Haji | Uteuzi wa Rais |
| 62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba. |
| 63.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope. |
| 64.Mhe. Mkongwe Nassor Juma | Nafasi za Wanawake. |
| 65Mhe. Moh'd Kombo Mkanga | Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 66.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja. |
| 67.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake. |
| 68. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | Uteuzi wa Rais |
| 69.Mhe. Omar Ali Jadi | Jimbo la Kojani. |
| 70.Mhe. Pembe Juma Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja. |
| 71.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu | Jimbo la Muyuni. |
| 72.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake. |
| 73.Mhe. Said Khelef Ali | Jimbo la Bumbwini. |
| 74.Mhe. Salim Abdulla Hamad | Jimbo la Mtambwe. |
| 75.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni. |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni. |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde. |
| 78.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Nafasi za Wanawake. |

| | |
|---|---|
| **Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim** | **Katibu wa Baraza la Wawakilishi.** |

**Kikao cha Sita – Tarehe 27 Januari, 2010**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba kuhusu Ripoti ya Uchunguzi wa Ajali ya Meli ya LCT Fatih.

**Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niwasilishe mezani hotuba ya maoni ya upande wa upinzani kuhusu Ripoti ya Uchunguzi wa Ajali ya Meli ya LCT Fatih. Naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 86**

**Ubakaji Kwenye Baa ya Kuuzia Pombe Kianga**

**Mhe. Ali Denge Makame** - Aliuliza:-

Kwenye Baa ya Kuuzia Pombe Kianga Mnamo mwezi wa Oktoba/Novemba, mwanamke mmoja alibakwa na kundi la watu. Tukio hilo lilisababisha mwanamke huyo kupoteza maisha.

Vyombo vya sheria vimechukua hatua gani ya kisheria zidi ya watuhumiwa wa tendo hilo?

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Kiongozi** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 86 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mnamo tarehe 09/11/2009 muda wa saa 02:24 asubuhi huko Kituo cha Polisi Mwera zilipokelewa taarifa za kuokotwa kwa mwanamke asiyejulikana kwa jina huko maeneo ya Nyampula akionyesha dalili za kubakwa na kuingiliwa kinyume na maumbile.

Mhe. Spika, polisi walifika mara moja kwa ukaguzi na kuthibitisha kutokea kwa tukio hilo la mwanamke ambaye aliyekuwa hajitambui alikuwa amelala pembeni mwa barabara na pembeni yake kukiwa na boksi la kondom, chupi na viatu alivyokuwa amevaa. Aidha, mwili wake ulikuwa na majeraha sehemu za kichwani, shingoni na kwenye mikono.

Mhe. Spika, majeruhi alipelekwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa matibabu ambako alilazwa akiwa huko alipata nafuu na tarehe 12/11/2009 aliweza kutoa maelezo kwa polisi wa upelelezi waliokwenda kumuhoji kwa ajili ya tukio hilo.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya ninasikitika kusema kuwa mwanamke huyo akiwa anaendelea kupata matibabu, siku tarehe 4/12/2009 alifariki dunia kwa kile daktari alichokieleza kuwa ni kifo hicho kilitokana na kujeruhiwa kwa uti wa mgongo *"Spinal Injury"*. Ni kwa bahati mbaya pia kuwa hadi mauti yanamkuta marehemu alikuwa bado kuwatambua waliomfanyia uhalifu huu, pengine hali ya upelelezi wa shauri hili ungekuwa na sura tofauti na ilivyo hivi sasa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu pahala pema peponi. AMIN.

**Mhe. Ali Denge Makame:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa masuala haya mara nyingi yanapotokezea chanzo chake kikubwa huwa kinaanzia kwenye klabu za pombe za kienyeji ambapo hawajasajiliwa na wala kuwa na leseni zilizokuwa halali.

Je, wizara yake inawaambia nini wananchi kwa mule mwenye klabu kama hivi ambapo mnauzwa pombe za kienyeji bila ya kusajiliwa ili kuvifanyiwa utaratibu wa kuvihamisha au kuvichukuliwa hatua yoyote ya sheria ili kupunguza matatizo haya, sijui anawaambia nini wananchi kwa ajili ya kupunguza tatizo kama hili?

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Kiongozi:** Mhe. Spika, suala la kuanzishwa kwa vilabu vya pombe katika maeneo ambayo sio rasmi hili ni suala ambalo wananchi wenyewe kwanza katika ile shehia huwa wanatakiwa suala lile waripoti kwa Sheha na kumuomba Sheha kuwa klabu kile cha pombe kifungwe. Pia, tumejaribu kuwashajihisha wananchi kwamba ruhusa ipo na kuna Mahakama ya Vileo, wananchi wakishajikusanya na wakenda kwa Sheha wakatoa malalamiko yao na wakaweka saini zao basi kesi ile huwa inapelekwa katika Mahakama ya Vileo na baadae hatua za kisheria kuchukuliwa.

Mhe. Spika, ni kwamba bado tunasisitiza kusema kwamba serikali bado hairuhusu katika maeneo ambayo hayakuwekwa maalumu kama ni vilabu kwa utaratibu wa kuweka kama ni vilabu vya pombe, suala hilo bado tunaomba sana

Masheha wasiruhusu watu kwa sababu sasa hivi kuna mtindo kama mtu amejenga nyumba yake ya kuishi, lakini baadae chumba kimoja anafanya ndio cha kuuzia pombe na vitu vyengine kama hivyo. Kwa hivyo, huu unakuwa sio utaratibu inatakiwa klabu ijengwe kama klabu na inatakiwa utaratibu wake tokea inapojengwa vile vibali vinaombwa basi viwe vinaeleza rasmi kama hapa tunajenga baa.

Kwa hivyo, hata ile taasisi ambazo zinazotoa vile vibali inajua kama eneo hili kwa kuangalia mazingira ya lile eneo hata wakitoa vibali haitoleta madhara katika eneo husika. Kwa hivyo, bado tunawaomba wananchi kama ziko baa kama hizo wasitumie nguvu na wala wasichukue sheria mikononi mwao isipokuwa wawasiliane na Masheha na kwa sababu tayari kuna watu walikuja wakalalamika na Masheha tukawaelekeza wakasimamia na vilabu hivyo baadhi yao vilifungwa. Hivyo, tunawaomba wananchi wengine wafuate mfano wa wenzao.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, Mhe. Waziri wanasema walipata fursa ya kumuhoji marehemu kabla hajafariki na mpaka dakika za mwisho alishindwa kuwatambua waliomfanyia vitendo vile. Je, ni hatua gani zilichukuliwa kwa hicho klabu cha pombe ambacho kilikuwa kinahusishwa ikiwa ni pamoja na kukifunga na kuwakamata wahusika wa hiyo baa na kuwahoji ili upatikane ule ukweli na ikiwa hawakuhusika upelelezi ukimaliza ingekuwa imetosheleza?

b) Je, baa hiyo ilikuwa ina kibali na kwa sababu zamani Mhe. Spika, mimi nakumbuka kuna jina moja kama sikosei na kama nitakosea naomba radhi kuna jina nilikuwa nalikumbuka lilikuwa linaitwa "*Wizidori*" ilikuwa askari wakifanya *patroo* sana maeneo ya Kwahani kwa sababu kulikuwa na hivyo vitu na baada ya kuwa mji wetu umekuwa kutokana na wageni wengi na maeneo ya Jang'ombe, pia yalikuwa yamo katika hiyo *patroo*? Kwa hivyo, Mhe. Waziri anapotwambia mpaka upeleke ripoti kwa Sheha kwanza, halafu ndio akaitwe polisi huoni hii ni moja ya sababu inayosababisha kwamba matukio haya yawe mengi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Kiongozi:** Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi alitaka kujua pamoja na kwamba marehemu alifariki kuna hatua gani nyengine ambazo zimechukuliwa baada ya hapo.

Mhe. Spika, mpaka sasa hivi bado uchunguzi unaendelea na kwa sababu marehemu mwenyewe hakuweza kumtaja muhusika. Kwa hiyo, ndio maana Jeshi la Polisi linakuwa liko makini sana ili wasije wakamtia hatiani mtu ambaye hakuhusika. Kwa sababu kama tunavyofahamu kama tunajitahidi sana kujaribu kufuata Utawala Bora na haki za binadamu. Kwa hivyo, upelelezi bado unaendelea mpaka sasa hivi na hatua zitakapofikia Mhe. Spika, baada huko mbele tutakuja kuwaeleza ni hatua gani ambazo zilizochukuliwa.

Mhe. Spika, vile vile, Mhe. Mwakilishi aliuliza kwamba klabu hiyo ina kibali au vipi? Ni kwamba hiyo klabu ina kibali na ndio maana huyo muhusika katika taarifa zake alisema alikuwa anatoka katika baa hiyo na ndio maana njiani akafikwa na huo mkasa. Kwa sababu huo mkasa haukumkuta hapo katika hiyo baa, huo mkasa umemkuta alipokuwa anarejea nyumbani na kama unavyojua katika mazingira ya saa nane za usiku na halafu mwanamke peke yake hayo ndio mazingira ambayo yaliyomkuta huko njiani.

Mhe. Spika, mimi kwanza nataka niwapongeze sana vijana wetu wa Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya hasa katika haya maeneo ambayo limetokezea hili tukio katika meneo ya Mwera.

Mhe. Spika, kuna operesheni maalumu huwa zinafanywa mara kwa mara kwa wale wapishi wa gongo na katika maeneo ambayo kuna watu sugu ni hii Wilaya ya Kati juu ya suala zima la upishi wa gongo. Mhe. Spika, ni kwamba tumeshaona na siku hizi kwa kuwa ndio watu wengi hawapati nafasi ya kuangalia televesheni kutokana na tatizo lililokuwepo, lakini tumeshashuhudia Jeshi la Polisi katika kituo cha Mwera wanakwenda wanamwaga madebe ya pombe na watu wanapelekwa Mahakamani na wanachukuliwa hatua za kisheria.

Mhe. Spika, ni kwamba suala alilozungumza Mhe. Mwakilishi kuwa hatuoni utaratibu wa kuvifunga vilabu hivi ni lazima wananchi watoe taarifa kwa Sheha na ule mtindo ambao waliokuwa wanautumia Jeshi la Polisi kuvamia si ungelisaidia zaidi.

Mhe. Spika, ni kwamba hizi baa ziko za aina mbili kuna baa zile ambazo zilizokuwa rasmi na zilizokuwa sio rasmi. Kwa mfano mtu kama nyumba yake anafanya baa huwezi kwenda ukamuhamisha bila ya taratibu. Kwa hivyo, ndio maana wanatakiwa waripoti kwa Sheha, wanajiorodhesha halafu hapo Sheha anafanya mkutano na wanapinga jambo lile kufanyika baadae hiyo kesi ndio inakwenda kwenye Mahakama ya Vileo na wananchi wanatakiwa waende wakatoe ushahidi wathibitishe kwamba ile baa hawaitaki. Kwa hivyo, haya maeneo ya kuvamia ndio zile tabu ambazo wapishi wa gongo wanapika saa

nane za usiku kwa hiyo pengine wananchi wamelala huku watu wanakoroga pombe. Kwa hivyo, hayo ndio maeneo ambayo polisi wanatakiwa waende ghafla kwa ajili ya uvamizi.

**Nam. 73**

**Njia Mpya ya Umeme kwa Ajili ya Kisiwa cha Unguja**

*Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa.*

**Nam. 37**

**Bodi ya Tiba na Dawa Asilia**

**Mhe. Hija Hassan Hija** – Aliuliza:-

Mhe. Spika, katika kuhakikisha usimamizi mzuri wa majukumu yake, SMZ imepitisha Sheria ya Usimamizi wa Tiba na Dawa Asilia pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Aidha, Bodi ya Tiba na Dawa Asilia tayari imezinduliwa rasmi. Vile vile, Mhe. Waziri amekwisha kutunga kanuni.

a) Zipo taarifa kwamba tangu Bodi hiyo kuzinduliwa haijafanya vikao vyake ambapo ilitakiwa kufanya vikao kila baada ya miezi mitatu. Je, hilo ni kweli.

b) Bodi ya Tiba na Dawa Asilia imeanzisha Kamati mbili, Kamati ya Utafiti na Kamati ya Wataalamu. Je, ni utafiti gani uliofanywa na kamati hizo tangu kuanzishwa ili kuwawezesha wananchi kufaidika na aina mpya za Tiba na Dawa Asilia.

c) Miongoni mwa changamoto zinazoikabili Bodi ni pamoja na fedha. Je, Mhe. Waziri unaweza kutupatia mchanganuo unaoonyesha mtiririko wa upatikanaji wa fedha ndani ya Bodi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 37 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, si sahihi kuwa tangu kuundwa kwa Bodi ya Tiba na Dawa Asilia halijafanya vikao vyake, bodi hiyo imezinduliwa rasmi mwezi wa Juni, 2009 na tayari limeshafanya vikao viwili na mkutano mmoja mkubwa kati ya bodi na waganga pamoja na watafiti mbali mbali wa tiba asili. Kikao cha mwanzo

kilifanyika tarehe 5 Juni, 2009 na kikao cha pili kilifanyika tarehe 5 Januari, 2010. Aidha, mkutano mkubwa ulifanyika tarehe 22 Agosti, 2009.

Mhe. Spika, bodi hii bado ni changa na hupata fedha kwa njia ya ada na usajili wanaotozwa waganga na wataalamu mbali mbali. Aidha, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imetoa fedha na bodi limefanikiwa kuwa na afisi zake na kuweza kununua samani na baadhi ya vitendea kazi. Hivi sasa bodi hiyo katika mkakati wa kuendeleza masuala ya utafiti tayari mtaalamu wa utafiti amepatikana katika Wizara ya Kilimo ambaye anafanya utafiti wa miti na dawa asili za Kizanzibari. Wizara ya Afya inaendelea na mikakati ya kupata watafiti zaidi.

**Mhe. Najma Khalfan Juma:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa wananchi wengi wa Zanzibar huwa wanatumia dawa za asili na kwa kuwa kuna hiki kitengo maalumu cha kuzichunguza hizi dawa za asili kwa ajili ya matumizi bora ya wananchi wetu.

Je, kuna dawa zozote zilizovumbuliwa mpaka sasa hivi kwa maradhi husika na wananchi wakawa wameshaanza kuzitumia.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, mpaka sasa hatujapata dawa maalumu zinazoweza kutumika kwa maradhi kutokana na dawa hizi za asili. Hili ni kutokana kwamba ndio kwanza sasa hivi tumeanza utafiti. Kwa hivyo, tusifanye haraka tuache twende na utafiti taratibu ili tuweze kuzichunguza dawa zetu ili tuone watafiti wanatwambia dawa gani zinafaa kwa maradhi gani hapo ndipo tutatangaza dawa gani ili tuweze kuzitumia.

**Mhe. Moh'd Ali Salim:** Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c).

a) Mhe. Spika, wakati tukiwa kwenye kamati katika Wizara hii ya Afya na Ustawi wa Jamii nilizungumzia hospitali iliyopo Kokoni karibu na Kiponda. Je, hospitali hii imesajiliwa rasmi.

b) Kama imesajiliwa rasmi leseni yao ni yakufanyia kazi wapi mpaka wapi.

c) Utafiti wa dawa zao niliyoelekeza ufanywe. Je, umefanywa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, hospitali ya Kokoni mimi siitambui hasa, lakini kwa utaratibu naweza nikasema kwamba

hospitali ya Kokoni itakuwa ni hospitali hizi za kawaida kama hospitali nyengine za watu binafsi.

Mhe. Spika, kama ni hospitali lazima itakuwa imepata usajili. Mhe. Spika, pia madawa hayo kama sisi tuna kitengo cha Wizara ya Afya hatujafanyia utafiti kama ni dawa za asili, hatujafanyia utafiti kama itakuwa ni dawa kama zinazotolewa kwenye mahospitali yetu itakuwa zimefanyiwa utafiti, lakini kama ni dawa za asili hatujafanyia utafiti kupitia kitengo chetu cha dawa asili.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nimemsikia Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali lake alisema kwamba hakujafanywa utafiti wa kina kuhusu hizi dawa zetu za asili kujua ipi inafaa na ipi haifai. Vile vile, ukiunganisha swali alilouliza Mhe. Moh'd Mula, kuhusu hiyo hospitali iliyoko Kokoni ni kuwa iko na inatumia madawa ya asili.

Mhe. Spika, wakati dawa yoyote ni sumu, lakini ukiitumia zaidi ya kiwango chake lazima itakuletea madhara na kwa sababu kuna sehemu kadhaa wako watu wanauza dawa hizi za asili na utumiaji wa dawa unataka vipimo vyake na uwe wa kitaalamu. Sijui Mhe. Naibu Waziri haoni kuwa ni hatari kwa hospitali hizi zinazotumia dawa za asili kutoa dawa ambazo wizara wenyewe haina uhakika wa kuwa inafaa au haifai wakati dawa ni sumu?

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, nataka kusema hatari ya dawa katika suala lake amesema kwamba hospitali hii inatumia dawa asili na hatuoni kuwa hizi dawa zinazotumika, kama hazijafanyiwa utafiti ni hatari.

Mhe. Spika, kwanza nataka kusema kwamba dawa yoyote ikitumiwa vyenginevyo ikiwa ya hospitali au sio ya hospitali matokeo yake ni hatari kwa sababu dawa yoyote ni sumu. Kwa hivyo, kama ni ya hospitali au sio ya hospitali matumizi ndio yanayotegemea, kama matumizi yakiwa mabaya kwa hivyo hiyo dawa inakuwa ni hatari kwa mtumiaji.

Mhe. Spika, labda niseme katika suala zima la adhma ya kuanzisha hii Bodi ya Tiba na Dawa Asili hapa nchini kwetu. Mhe. Spika, haya sisi wizara yetu tumeyaona na ndio maana tukaona ili kujikinga kwa matatizo mbali mbali madawa yanayotumika ovyo, hayana vipimo, hayana viwango, hatujui matatizo yake yakoje. Kwa hivyo, ndio tukaamua wizara yetu ni bora tuanzishe hiki kitengo cha tiba asili ili kiende na utaratibu pamoja na utaalamu wa sasa unavyokwenda. Kwa sababu hizi dawa ndio zinatumika sana ndio tukasema kwa utaratibu unaotumika hapa nchini sio vizuri kwa utaratibu huu

tunaokwenda nao. Kwa hivyo, hao wote itakapofika wakati itabidi dawa zao zipimwe ili zionekane zinakubalika kutumika kwa mujibu wa taratibu za vipimo na viwango vinavyotakiwa.

**Nam. 39**

**Ujenzi wa Nyumba za Madaktari**

**Mhe. Hija Hassan Hija** - Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi zake pamoja na Washirika wa Maendeleo kwa uamuzi wao wa kuwapunguzia wananchi kero za upatikanaji wa huduma za afya kwa kuwajengea nyumba za madaktari katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

(a) Ni kampuni ngapi ziliingia katika mchakato wa maombi ya ujenzi wa nyumba hizo.

(b) Ni kampuni gani inayojenga nyumba hizo na ni kwa gharama za kiasi gani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii** - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 39 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Zabuni za ujenzi wa nyumba 40 za wafanyakazi vituoni pamoja na vituo vya afya 6 Unguja na Pemba ilitangazwa tarehe 14/7/2008. Jumla ya wakandarasi 6 walichukua zabuni kwa ujenzi wa Unguja na 3 kwa Pemba.

Waliochukuwa zabuni kwa ujenzi wa Unguja walikuwa ni wafuatao:-

1. *Mazrui Building Contractors Ltd.*
2. *RANS Building Company Ltd.*
3. *Tanzania Building Works.*
4. *Sinani Building Contractor Ltd.*
5. *China Railway Jianching Engineering Co Ltd.*
6. *Nadhra Engineering and Construction Ltd.*

Waliorejesha zabuni ni:-

1. *Mazrui Building Contractors Ltd.*
2. *RANS Building Company Ltd*
3. *Nadhra Engineering and Construction Ltd.*

Waliochukua zabuni kwa Ujenzi wa Pemba walikuwa ni:-

1. *Mazrui Building Contractors Ltd.*
2. *RANS Building Company Ltd.*
3. *Tanzania Building Works*

Waliorejesha zabuni ni:-

1. *Mazrui Building Contractors Ltd.*
2. *RANS Building Company Ltd.*

b) Mhe. Spika, mjenzi wa Pemba ni *Mazrui Building Contractor Ltd* kwa gharama ya shilingi 3,926,328,987.04, Mjenzi wa Unguja ni *RANS Building Company* kwa gharama ya shilingi 3,566,780,957.04. Jumla ya gharama kwa Unguja na Pemba ni 7,493,109,944.08 ambazo zote zimelipwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*)

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Spika, naomba kujua ni sababu zipi za kitaalamu zilizopelekea nyumba hizo kujengwa na wakandarasi wawili tofauti, mmoja Pemba na mwengine Unguja.

(b) Baadhi ya nyumba ambazo zimejengwa ziko katika visiwa, kama Shamiani Mwambe na Makoongwe Mkoani Pemba na hadi sasa hakuna huduma ya umeme. Kwa kuwa nyumba hizi ni za kisasa kuna hatua gani za makusudi za wizara za kuzipatia nyumba hizi huduma za nishati ili kuweka mazingira safi na ustawi wa nyumba zile.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, kwanza utaratibu wote wa *tender* umefuatwa kwa Unguja na Pemba. Kwa hivyo, kwa Unguja amepata *RANS Building Company* na kwa Pemba *Mazrui Building Company*.

Kwanza, yalitoka matangazo kwenye magazeti, watu wakachukua zabuni ikendazake mpaka zikapelekwa Makao Makuu ya Tunis na wao wakasema

*letter of no objection*. Kwa hivyo, waliobarikiwa kwa Unguja ni *RANS* na kwa Pemba ni Mazrui. Utaratibu wote umefuatwa hakuna kilichofishwa. Hilo la kwanza.

Pili, tunafanya mipango kwamba haya maeneo ya visiwa ambayo hakuna umeme tuweze kufanya mpango wa kuweka *solar power*. Hayo mambo tumeyaandaa, lakini tukifanikiwa basi sehemu zote hizo zitakuwa na huduma za umeme wa jua.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi alisema kwamba katika zabuni ya Pemba kuna kampuni tatu ambazo zilijitokeza kuomba. Lakini kwa mujibu wa marejesho ni kampuni mbili ambazo zimerejesha. Sasa swali langu ni kwamba, kwa mujibu wa taratibu wa *tender* za kiserikali kampuni ambazo zinatakiwa zirejeshe ni tatu na kama kutatokezea kwamba zimerejesha mbili basi *tender* ile itangazwe tena upya. Je, wizara yake imefanya hivyo.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, kwa Pemba baada ya kutolewa tangazo waliojitokeza kuchukua zabuni kwanza walikuwa watatu, *Mazrui Building Contractors, RANS Building Company na Tanzania Building Works.* Waliorejesha ni *Mazrui Building Contractors* na *RANS Building Company.* Kwamba watatu ndio hawakujitokeza, wamejitokeza wawili, ni kwamba sisi tukishakupata vitu kama hivi tunapeleka Makao Makuu ya *ADB*, Tunis

. Kwa hivyo, wao ndio watakaosema kwamba hawakubaliani na *tender* hiyo, lakini wao wamekubali na wameleta *letter of no objection* tukatia mkataba kwa Pemba amepata Mazrui tukamkabidhi kazi na kazi inakwenda vizuri, ujenzi unakwenda vizuri na tunatarajia karibuni nyumba hizo tutakabidhiwa 20 za Pemba pamoja na hospitali baadhi yake kama za Konde na sehemu nyenginezo.

**Nam. 59**

**Marekebisho ya Sheria ya Bima**

**Mhe. Ali Abdalla Ali** – Aliuliza:-

Sheria ya kuanzisha Bima Tanzania 1996 imefanyiwa marekebisho makubwa kwa lengo la kuleta ufanisi mzuri. Miongoni mwa marekebisho hayo ni kuweka kianzio cha mtaji wa Bima kuwa shilingi bilioni moja na kuondoa utaratibu wa kukopesha Bima.

(a) Je, Mhe. Waziri utaratibu huu mpya umeleta mafanikio gani mpaka sasa.

(b) Je, Shirika letu la Bima za Zanzibar litaweza kuukabili ushindani ukizingatia wingi wa Makampuni yanayowekeza kwenye biashara hii.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 59 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba sheria ya Bima Nam.18 ya mwaka 1996 imefanyiwe marekebisho makubwa na kuwekwa badala yake sheria mpya ya Bima Nam.10 ya mwaka 2009.

Mhe. Spika, sheria hiyo kwa sasa imetumika kwa muda mdogo tangu yapitishwe mabadiliko hayo makubwa. Kwa hivyo, ni vigumu kuweza kupata tathmini au kupima mafanikio yake. Tutaweza kupima mafanikio angalau baada ya kutumika kwa mwaka mmoja hivi.

1. Makampuni ya Bima ambayo yamesajiliwa Tanzania ni 26, wingi wa makampuni ya Bima yanafanya kuwe na ushindani mkubwa sana wa kibiashara. Kwa upande wa Shirika la Bila la Zanzibar tayari wameweka mikakati mbali mbali kuweza kukabiliana na ushindani huo wa soko kama ifuatavyo:-

- Kurekebisha muundo wa shirika ili kuweza kupunguza gharama za uendeshaji kila inapoyumkinika.

- Kupunguza wafanyakazi ambao hawana sifa na kuweza kuajiri wengine wenye sifa zinazohitajika kuweza kukabiliana na ushindani mkubwa wa kibiashara uliyopo.

- Kufungua matawi katika afisi za kanda Tanzania Bara ili kuweza kuongeza wigo wa soko. Uzoefu unaonesha kwamba, hivi sasa mapato ya kanda yanapanda kila mwaka, hali inayoashiria kukubalika kwa *Zanzibar Insurance Company* Tanzania kote.

- Kuweka mpango kazi wa miaka mitatu ili kuwa na mipango ya muda mrefu.

- Kuboresha huduma zake kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

- Kuifanya bora zaidi mikataba na viwango vya Bima ili viendane na mahitaji ya soko.

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri amekiri kwamba hivi sasa ushindani wa biashara ya bima ni mkubwa na tayari nchi nzima imefunguliwa matawi 26.

Je, hapa petu Zanzibar matawi mangapi yamefunguliwa. Hilo la kwanza.

La pili, pia katika mchakato wao bima hapa petu wameondosha mkopo wa bima lazima ukate *cash*.

Je, Mhe. Waziri haoni kuwa hiyo ni sababu moja ya kuweza kupunguza mapato na wateja, wakati biashara ya sasa hivi ni kukopa na *cash*.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, ninayo orodha ndefu ya hayo matawi au kampuni 26, lakini sikuyaweza kuya-*categorize* ngapi ziko Zanzíbar. Naomba hili nilichukue nitajaribu ku-*categorize* ngapi ziko hapa halafu nitamjuilisha.

Kuhusu kukopa na kulipa, ni kweli anavyosema Mhe. Mjumbe kwamba biashara ni kukopa na kulipa. Lakini naomba nimhakikishie si kwa bima, kwa sababu mambo ya bima tunayajua. Mara nyingi huwa tunalalamika kwamba hatupati haki zetu madai yapo halisi lakini wagumu, kutokana na sababu hiyo. Wako wale majenti wao ndio wanalikopa hilo shirika, sasa wao mara nyingi hawalipi, wanatuzungusha sana. Sasa sisi tunajaribu sana kuondoa huo mwanya wa kukopa na kulipa. Wao kama maajenti wetu basi wachukue ahadi za ukweli watulipe. Hivi sasa tunawadai pesa nyingi tu. Kwa hivyo, kwa biashara hiyo kwa hapo hai-*apply* Mhe. Spika, ahsante.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Nakushukuru Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kufuatia marekebisho haya ya sheria hii ya mwaka 1996, shughuli za Bima zimefanywa chini ya usimamizi wa Kamisheni ya Bima ya Muungano. Kwa kuwa chini ya usimamizi huo Shirika la Bima la Zanzíbar limetakiwa kuuza rasilimali zake ambazo zilikuwa zinamiliki na pia kuzuwiwa kununua baadhi ya nyengine.

(a) Utaratibu wa kuziuza rasilimali ambazo Shirika la Bima la Zanzíbar linazimiliki hapa Zanzíbar unafuata utaratibu gani.

(b) Kwa sababu Shirika la Bima la Zanzíbar linahitaji sana kununua na kumiliki afisi pale Dar es Salaam, jamba ambalo Kamisheni ya Bima ya Tanzania imezuia kwa kulinda ile inayoitwa *sovereigncy margin* ya Shirika la Bima la Zanzíbar. Je, serikali kama mmiliki wa Shirika la Bima la Zanzibar ina mpango gani wa kununua jengo ambalo yenyewe ndio itaweza kulikodisha Shirika la Bima kwa bei muwafaka.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, utaratibu unaofuata katika uuzaji wa mali hizo ambazo zinaonekana kama za ziada kwa shirika ni kutangaza katika magazeti na yule *highest bidder* ndiye anayeuziwa. Huo ndio utaratibu wa utandawazi.

Pili, afisi mpya Dar es Salaam. Ni kweli kwamba tumekuwa tukikodi afisi ya Dar es Salaam kwa pesa nyingi, kwa kweli shirika limeshaandaa utaratibu wa kutafuta kiwanja kuweza kujenga afisi yake, lakini bado hatujafanikiwa. Unajuwa biashara yoyote iko mjini, sasa ukipata kiwanja nje ya mji kidogo ni vigumu. Tunajua sote bei za viwanja katikati ya mji zilivyo ghali, chukulia hapa kwetu tu, maeneo ya darajani mabenki mengi yalipojikita mpaka vikokotoni kuweza kupata kiwanja au nyumba sehemu hiyo.

Kwa hivyo, tunajitahidi tuweze kupata afisi mpya na ya kileo ambayo ina heshima ya biashara ya bima. Utakuta hata majengo yetu mengine yaliyoko Mwanza na Arusha, kwa kweli yako mwahala yanajitangaza yenyewe kwamba hapa kweli nakwenda kwenye afisi ya bima, lakini huwezi kuweka afisi ya bima kichochoroni ambapo hapana heshima yake. Kwa hivyo, wazo lake Mhe. Said Ali Mbarouk ni zuri na linafanyiwa kazi na shirika.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Hapo miaka ya nyuma kidogo Shirika la Bima lilitaka kukumbana na misukosuko hasa kutokana na wale mawakala wajanja na ilipelekea shirika hilo kidogo kutaka kupoteza mwelekeo. Hivyo, mawakala kama wale siku hizi wizara yake imewachukulia hatua gani.

Pili, Tanzania ina zaidi ya mashirika 26 ambayo inashindana na Shirika la Bima la Zanzíbar. Je, Shirika la Bima la Zanzíbar katika soko hapa Tanzania lina nafasi ya ngapi.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, kuhusu mawakala kuwa tumewachukulia hatua gani, hatua ya kwanza kabisa ni kuwazuilia ule uwakala wetu kwao. Lakini hatuwazuilii tu halafu tukawaachia, tunataka zile pesa zetu tunazowadai lazima zirudi. Taarifa nilizonazo kwa

Tanzania kwa ujumla tunawadai zaidi ya shilingi milioni mia tisa. Juzi tu mwenyewe nilifanya ziara kutembelea maofisi yao yote Dar es Salaam, Mwanza mpaka Arusha na nikaona zile kazi wanazofanya.

Pia, Mhe. Ame Mati, aliuliza tuna nafasi gani. Kupanga kwamba wa kwanza, wa Pili,na wa watatu hatujaweza, lakini ninachotaka kusema kwamba Shirika la Bima la Zanzíbar limejitangaza vizuri na limepata sifa kubwa sana na niseme kwamba watu wengi sasa au makampuni makubwa mengi yaliyoko Bara yameanza kuona ukweli. Kwa sababu unajuwa Mashirika ya Bima mengine nitumie nene si zuri lakini labda *the write word* si wababaishaji, yaani kweli kama haki yako ipo wanakulipa.

Lazima nitoe pongezi kwa makampuni mengine ya Wazanzibari ambao kwa kweli ni makubwa Tanzania na wamejiandikisha katika shirika hili. Shirika moja kubwa sana ni hili la *Zanzíbar Milling Co-operation* la Bwana Bahkresa pamoja na meli zake na biashara zake zote ameziandikisha kwenye Shirika la Bima la Zanzíbar. Kwa kweli iko haja ya kumpongeza sana na yeye anamiliki *fleet* ya magari zaidi ya 15,000 na yote ameyasajili kwenye Shirika la Bima la Zanzíbar. Utaona mfano vipi shirika letu linathamini.

Lakini pia, nilitembelea baadhi ya makampuni Mwanza makubwa tu mengine ya wajenzi na wote wanaacha kampuni nyengine, sababu yao kubwa wanapodai wanasumbuliwa nakuhangaishwa, lakini Shirika la Bima la Zanzíbar kwa kweli panapostahiki wanalipa haki zao. Kwa hivyo, tuna heshima kubwa sana kwenye biashara hiyo.

**Nam. 60**

**Utaratibu wa Kukusanya Mapato Tanzania**

**Mhe. Ali Abdulla Ali** - Aliuliza:-

(a) Kwa kuwa kutumia kiwango cha juu na kiwango cha chini cha makadirio ya kodi husika yote ni halali kisheria, kwa nini *TRA* kwenye Bandari za Tanzania Bara hasa Dar-es-Salaam hudai kodi zaidi ili wafikie kiwango cha juu cha makadirio ya kodi hiyo kwa bidhaa fulani.

(b) Kwa kuwa uchumi wa Zanzibar ni mdogo na hutegemea sana kodi za forodha. Na kwa kuwa usawa wa viwango vya kodi baina ya Zanzibar na Tanzania Bara unaweza kuathiri ukusanyaji wa mapato na uchumi wa Zanzibar, kwa nini serikali yetu (SMZ) isipiganie kuwepo kwa mfumo wa kodi unaokubali viwango tafauti vya kodi za forodha ndani

ya taasisi moja ya utozaji kodi (*TRA*) kwa lengo la kunusuru uchumi wa Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 60 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kawaida katika nchi zote zenye mfumo wa Muungano kukubaliana juu ya kodi za mambo ya Muungano na maeneo mengine kwa ajili ya serikali zinazoshiriki katika Muungano huo. Kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa Hati ya Muungano na baadae Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Kodi za Muungano ni Ushuru wa Forodha, Ushuru wa Bidhaa zinazozalishwa nchini na Kodi ya Mapato ya Makampuni na watu binafsi.

Kwa kuzingatia kuwa nchi mbili hizi ndio zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuzingatia kuwa ushuru wa forodha ni jambo la Muungano, pia kwa kuzingatia matakwa ya itifaki ya soko la pamoja la Afrika Mashariki, hakuna viwango tofauti vya ushuru wa forodha baina ya Tanzania Bara na Zanzíbar. Utozaji kodi unaolalamikiwa na wafanyabiashara wa Zanzíbar wanapoingiza bidhaa zao Tanzania Bara unatokana na utaratibu wa tathmini wa bidhaa.

Kumekuwa na madai kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania kwamba thamani inayokubaliwa katika bandari za Zanzíbar ni ndogo na hivyo kupunguza mapato ambayo yangeweza kukusanywa. *TRA* Tanzania Bara wanarekebisha thamani hiyo na kudai tofauti ya ushuru baina ya ule uliolipiwa kwa thamani ya chini hapa Zanzíbar na ile inayoonekana kuwa ndio muwafaka kwa upande wa Tanzania Bara. Hayo ni madai ya *TRA* Tanzania Bara.

Naomba nikiri kwamba utaratibu huu umekuwa chanzo cha malalamiko mengi kutoka kwa wafanyabiashara wanaohamishia vida kutoka Zanzíbar na kupeleka Tanzania Bara. Kwa maoni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar, utaratibu unaotumiwa na *TRA* Tanzania Bara kwa bidhaa kutoka Zanzíbar haufuati misingi ya tathmini ya vida inayotambuliwa na Shirika la Biashara la Kimataifa (*WTO*) na ile ya forodha (*WCO*).

Mashirika haya yanaongozwa na Mkataba wa Utathmini wa Forodha (*Agreement on Customs Valuation – ACV*) ambao Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeuridhia. Baada ya kushindwa kupatikana suluhu muwafaka kwa muda mrefu, suala hili liliwasilishwa katika Kamati ya Kujadili Kero Zilizopo

katika Muungano inayoongozwa na Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumshirikisha Mhe. Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na wataalamu wengine.

Kamati hii maalumu ya kulishughulikia suala hili imekamilisha kazi yake na inatarajiwa kujadiliwa hiyo ripoti hivi karibuni na Wizara za Fedha za pande mbili hizi kabla ya kuwasilishwa tena katika Kamati ya Mhe. Makamu wa Rais.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa ushuru wa forodha ni sehemu muhimu ya mapato ya SMZ, mchango wake katika mapato ya serikali umeshuka sana kwa miaka kumi iliyopita kutoka wastani wa asilimia 66 za mwaka 1999/2000 hadi wastani wa asilimia 33 mwaka 2008/09. Kwa kuwa kwa ujumla mapato ya serikali yamepanda sana katika kipindi hicho, kushuka huku kunapaswa kuonekana kama ni mafanikio katika upanuzi wa uwekezaji wa ndani na hivyo kuwa chanzo muhimu cha mapato ya serikali.

Hata hivyo, serikali inatambua umuhimu wa kuwa na upeo mpana zaidi wa kusimamia sera za kodi zikiwemo ushuru wa forodha. Kwa dhamira hii, serikali inaendelea na juhudi za kufanya utafiti wa namna na uyakinifu wa kuifanya Zanzibar kuwa eneo muhimu la kiuchumi ndani ya Itifaki ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (*Special Economic Zone – SEZ*). Matokeo ya utafiti huu yanaweza kupelekea Zanzibar kuwa na fursa ya kuwa na sheria maalumu zikiwemo za forodha.

**Mhe. Asha Moh'd Hilal:** Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Hawa ndugu zetu wa Tanzania Bara kuhusu suala hili wao walikubaliana pamoja na sisi kusema watatumia *computerise*, lakini mpaka leo tunatumia *computerise* na ushuru walioutaka ndio tunaoweka na bado wanaendelea na mfumo wao huo huo. Je, Mhe. Waziri huoni kwamba hawa ndugu zetu wana njama ya kuzidi kutumaliza.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, nafikiri mara nyingi niliwahi kueleza kwamba kuweka utaratibu ni suala moja na kufuata utekelezaji wa utaratibu ule ni suala la Pili. Mara nyingi suala hili tumelizungumza, tunafika tunakubaliana baada ya mwezi mmoja au miwili tunarudi pale pale, ndio maana tukasema safari hii tulichukue mpaka tufike mahala tuweke kama sheria hasa, nafikiri hapo tena itatusaidia sana. Kwa sababu tukiweka tu tukakubaliana, kwa mazungumzo tu naona hatufiki mahala, lakini kufikia huko tumeunda hiyo kamati maalumu kuweza kufanya tafiti ya haya mambo kuona matatizo yake na wakachukuliwa wataalamu wetu wa Zanzíbar na wa Tanzania Bara, wakakaa pamoja wakafanya utafiti, wakawahoji

wafanyabiashara wa Zanzíbar, wakapitia taratibu zetu za hapa *TRA* Zanzíbar, wakenda zao Dar es Salaam wakaona vipi wanafanya kazi na sehemu nyengine *TRA* zinakokusanya kodi.

Sasa kama nilivyosema hiyo ripoti tayari imeshakamilishwa na karibu tutaijadili kwanza sisi katika wizara zetu za fedha na baadae kuweza kutoa mapendekezo yetu.Nakubaliana na anayosema Mhe. Asha Moh'd Hilal kwamba kweli kuna wakorofi ambao makusudi wana lengo la kutuzamisha. Kwa sababu kila wanapoona biashara imenona au imekubali ya magari basi wanajaribu kutuzamisha makusudi. Kwa hivyo, kauli yake mimi naikubali kwamba kweli inaelekea wapo watendaji, si wote, lakini wapo baadhi ya watendaji wakorofi wanafanya makusudi kutudhalilisha.

**Mhe. Juma Duni Hají:** Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza madogo tu. Ninachoamini kwamba wafanyakazi wa *TRA* waliyopo Zanzíbar ni sehemu ya wafanyakazi wa *TRA* wa Tanzania nzima. Sasa je, inamaana hawa wa Zanzíbar tu ndio waliokuwa hawaaminiwi kufanya tathmini sahihi. Kwa sababu mipaka ya kutizama vitu vinavyoingia haipo Zanzíbar tu, kuna Tanga, kuna kila penye mipaka kati ya nchi yetu na nchi nyengine kuna forodha, lakini kila mara kwetu tu ndio tunafanya thamani chini kwengine hakufanywi hata ikawa ni miujiza. Hilo la kwanza.

Lakini la pil, Mhe. Waziri alieleza hapa kwamba mapato yetu ya forodha yameshuka sana na anasema pengine ni kwa sababu ya kuongezeka kwa uwekezaji ndani. Hivyo, Haoni ni kwa sababu kwamba uagiziaji ndio uliyoshuka na usafirishaji pengine wa zao letu la karafuu nao vile vile umeshuka.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) (MBLM) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, hii aliyozungumza yeye ndio *observations* za *TRA*, sisi kama SMZ tunasema hapana. Sasa huo ni ukweli kwamba kuna kutokubaliana kwa sababu hao *TRA* Zanzibar mabosi wao wote wanatokea Tanzania Bara na wapo hapa hapa. Sasa kama wanafanya *under valuation* hapa wanakuwa *supervised* na nani, si hao mabosi wao. Kwa hiyo, hapo ndio kwenye huo ubishi kwamba wao wanadai hivyo, lakini sisi hatukubaliani nao. Ndio tukasema wacha tuzungumze tutumie nguvu ya hoja tuone mpaka tutakapofika katika suala hili.

Kwa hiyo, naomba mtuamini, nafikiri nyote mtakubaliana na muda mwingi tunaokuwa tukizungumza suala hili, lakini kwa kweli wenzetu hawa wa *TRA* niseme kama hawatuamini, huo ni ukweli kwa sababu tunazungumza, tunakubaliana, wanakuja, wanarudi, wanafanya wakati mwengine *surprised checks*, wanakuja hapa wanapata labda *tip* wanacheki, lakini wakirudi uzi ule

ule. Lakini naamini tulipofika hapa sasa katika mazungumzo na hasa hii ripoti nafikiri itatuweka pazuri.

Kuhusu usafirishaji kama nilivyosema kwamba kwa ujumla ninapozungumza nafikiri Mhe. Juma Duni Haji, nazungumzia mapato ya *TRA na* sio mapato mengine, yaani sijumuishi karafuu na kwengine. Hapa tunapozungumza mapato ya *TRA* zaidi tunakusudia kuna *domestic revenue,* hizi *customs duty* na nyenginezo. Huko mambo ya karafuu *export* zile ni mbali. Kwa hiyo, haya tunashukuru kwamba wamekuwa wakiagiza hapa na kama nilivyosema *investment* imeonekana kuwa kubwa, sasa kuagiza kutoka nje labda Tanzania Bara au wapi kumepunguka. Lakini kwa sasa hivi tumejitanua kwa sababu wanaagiza hapa hapa na *investment* kwa kweli imekuwa kubwa.

**Mhe. Spika:** Niwaombe radhi Waheshimiwa Wajumbe swali limechukua muda mrefu kidogo tuendelee na swali jengine.

**Nam. 35**

**Matatizo ya Hali ya Hewa Zanzibar**

**Mhe. Ali Suleiman Ali –** Aliuliza:-

Mhe. Waziri, Zanzibar imefaidika vipi na misaada ya kitaaluma na kifedha inayolenga kusaidia kupunguza athari zitokanazo na ongezeko la hali ya joto duniani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira –** Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu imekuwa ikifaidika na misaada ya kitaaluma na kifedha inayolenga kusaidia kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya hali ya hewa duniani. Kwa mfano Chuo Kikuu cha Turku cha Finland kinashirikiana na wizara yangu kufanya utafiti kuhusu taathira za mabadiliko ya hali ya hewa kwa upande wa mimea *(vegetation)* hapa nchini. Utafiti huo pia unaangalia namna gani mimea hiyo inaweza kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa inayoendelea hivi sasa.

Mhe. Spika, hivi sasa wizara kwa kushirikiana na Shirika la *CARE* Tanzania tumo katika majadiliano ya kuanzisha mradi wa pamoja utakaohusika na upunguzaji wa hewa ya mkaa *(carbondioxide)* itokanayo na ukataji na upoteaji

wa misitu ya asili, chini ya mpango *(programme)* inayoitwa *REDD (Reduce Emission from Deforestation and Forest Degradation).*

Mradi huu unatarajiwa kufadhiliwa na Serikali ya Norway. Pia, kwa kushirikiana na Mradi wa *MACEMP*, wizara imeweza kupunguza athari hizo kwa kupanda mikoko katika maeneo ya Unguja na Pemba kwa mashirikiano na Jumuia mbali mbali zisizo za Kiserikali *(NGOs).*

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mtikisiko wa hali ya hewa duniani umeathiri mambo mengi nchini kwetu na duniani kwa jumla. Wenzetu katika harakati hizi wamegeuza jina ambalo kidogo mimi linanipa mashaka wanasema tabia ya nchi. Kwa kuwa Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira alihudhuria mkutano huo. Je, suala hili ambalo linapigiwa kelele duniani sasa hivi kuhusiana na athari mbali mbali kwa ujumla. Hivyo, sisi Zanzibar tumenufaika na nini pamoja na yale aliyoyataja Mhe. Waziri katika mkutano huo ambao amehudhuria yeye .

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali hilo, wizara yangu inatengeneza taarifa ambayo itawasilishwa kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ili waweze kupata picha angalau ya hali halisi ya mkutano ule wa Denmark. Mle watapata mambo mengi sana pamoja na haya maswali wanayouliza sasa hivi.

Mhe. Spika, kwa kujibu swali, kwanza niijibu hii tabia ya nchi. Tabia ya nchi ni jina ambalo lililopewa tu katika huo mkutano, lakini kwa ufupi ni ile ile mabadiliko ya hali ya hewa duniani kwa hiyo tusibabaike.

Lakini la pili, kwamba Zanzibar tumefaidika vipi na mkutano huu. Kwanza labda niseme kwamba tumefaidika kupata elimu kuwa dunia sasa imekabiliwa na mabadiliko ya hali ya hewa makubwa tu, tena hali ya hewa hii imeikumba dunia nzima.

Mhe. Spika, *Professor* mmoja wa sayansi alisimama kule kwenye mkutano kuwaambia kwamba wasifikiri labda madola makubwa haya hayataathirika kutokana na hali hii ikiwa tutaendelea kuzidi kuharibu hewa.Kwa hivyo, ikitokea athari itakuwa ya dunia nzima, nchi tajiri na nchi maskini. Lakini bila shaka sisi nchi zetu zilizoendelea tutaathirika zaidi.

Kwa hivyo, kwa ufupi pale mjadala ukaendelea kwa urefu sana, lakini mwisho ikakubaliwa kwamba basi maazimio ama mapendekezo yaliyofikiwa katika mkutano huu wa Denmark yapelekwe katika mkutano utakaofanyika mwezi

Disemba nchini Mexico kwa kupata uamuzi. Maamuzi makubwa sana yaliyotakiwa ni kwamba nchi zinazozalisha sana gesi duniani ikiwa pamoja na Marekani, China na nyenginezo, wajaribu kupunguza hizi nyuzi joto zinazotokana na viwanda vyao kwa asilimia fulani. Hiyo katika mkutano utakaokuja wataweza kusema kwamba watapunguza kwa kiasi gani.

Inasemekana kwamba hivi sasa nyuzi joto duniani ni mbaya sana na hii ndio hali tunayoiona ya joto la kupita kiasi. Sasa hali hii ndio hayo mabadiliko ambayo wanataka wapunguze, yaani nyuzi joto hizi zipungue iwe hali kidogo ni afadhali.Kwa mfano hii ni muhtasari lakini zaidi ni kuwaletea ule warka Wajumbe wa Baraza lako watapata taarifa kamili. Lakini kwa upande wa Zanzibar kama nchi nyengine zote na sisi vile vile tunaathirika.

La kwanza, katika visiwa vyetu hivi kuna sehemu nyingi sana za Unguja na Pemba bahari inakula. Hii kwa upande wetu wizara tumewaambia Idara yetu ya Mazingira kuweza kufanya utafiti sehemu zote zinazohusika na waandike ripoti kamili pamoja na hatua gani zitakazoweza kukabiliana na hali hiyo. Ikiwa watatoa gharama hizo kubwa basi tutashirikiana na Serikali Kuu au kuomba misaada kutoka nchi marafiki mbali mbali waweze kukabiliana na hali hii.

Mhe. Spika, zoezi hilo limo katika kufanywa kuweza kujua mporomoko au kuliwa bahari katika visiwa vyetu uko katika hali gani.

Mhe. Spika, vile vile, hata katika mambo haya ya *irrigation* tumeathirika kwa sababu maji yamekuwa haba sana kutokana na wingi wa joto.

**Nam. 92**

**Mkutano wa Hali ya Hewa Copenhagen**

**Mhe. Hija Hassan Hija –** Aliuliza:-

Mnamo mwezi wa Disemba, 2009 nchi mbali mbali duniani zilikusanyika mjini Copenhagen, Denmark kuzungumzia mabadiliko ya hali ya hewa. Aidha, nchi za visiwa kama vile Maldives sauti zao zilisikika katika mkutano huo.

(a) Je, Mhe. Waziri, Zanzibar kama visiwa iliwakilishwa na ujumbe gani.

(b) Je, nini ilikuwa matokeo ya mkutano huo.

(c) Katika mkutano huo zaidi ya waandishi wa habari 3,500 walihudhuria. Je, ni waandishi wangapi wa Zanzibar walihudhuria mkutano huo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira –** Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 92 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba vifungu viwili nivijibu kwa pamoja kifungu (a) na kifungu (c).

Mhe. Spika, kwanza nataka nimhakikishie kwamba katika mkutano ule ambao ulifanyika Copenhagen, Denmark hakukuwa na mwandishi wa habari pamoja na kwamba Tanzania iliwakilishwa na waandishi wa habari kutoka *TBC*.

(a) Zanzibar iliwakilishwa na ujumbe ufuatao:

- Mhe. Waziri wa Kilimo, Katibu Mkuu – Wizara ya Kilimo.
- Afisa Mdhamini – WKMM Pemba.
- Mkurugenzi wa Mazingira, Mkurugenzi Idara ya Misitu.
- Mkurugenzi – Idara ya Kukabiliana na Maafa ambaye huyu anatoka katika Afisi ya Waziri Kiongozi.

(b) Matokeo ya mkutano huo yalikuwa ni kutoa tamko la kisiasa la kuanzishwa mkataba mpya wa kukubaliana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani. Matamko hayo yalitolewa na Wakuu wa Mataifa yaliyohudhuria mkutano huo ambapo Tanzania iliongozwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Ali Moh'd Shein. Aidha, ilikubaliwa kwamba makubaliano hayo yatapitishwa katika mkutano ujao ambao umepangwa kufanyika mwezi wa Disemba, 2010 *Mexico City* nchini Mexico.

Lakini Mhe. Spika, nawaomba wenzangu wakubaliane na mimi wale mashabiki zaidi wa *Manchester United* kwamba iliahirishwa mechi moja kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, hata pale Uingereza kulikuwa kuna hofu sana. Tumesema kwamba tunategemea sana mataifa nayo kuathirika sio kwamba sisi nchi masikini, kama kilivyo kifo hakipendelei basi na hali ya hewa haipendelei. Kwa hivyo, kila tukizidi kuchafua hali ya hewa tutaathirika sote.

Kule Ulaya zaidi pale Uingereza ilitokea baridi ambayo ilileta hofu na watu wamefariki na hata ndege nazo zilikuwa zimeondoka katika ule mwelekeo wake zilikuwa haziruki. Lakini pia, hata China ilianguka theluji nyingi sana

ikawaathiri wanafunzi na skuli zikafungwa. Kwa hivyo, hizo ni athari ambazo dunia sasa inaanza kuziona.

Kwetu sisi hapa Zanzibar tunajiona wenyewe, mbali ya kwamba joto limezidi sasa hivi hujui unatembea nje au unatembea ndani, sijui ukae wapi na kutembea vyenginevyo sisi Wazanzibari hatuwezi. Yaani ile nusu uchi hatuwezi kwenda kama hivyo, sisi utamaduni wetu lazima tuvae vizuri na tujistiri. Kwa hiyo, tunakabiliana na hiyo hali ya hewa.

Lakini pia, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kama tunavyosema siku zote, tuchukue juhudi ya makusudi kuweza kupanda miti kwa wingi ili tuweze kuirejesha hali ya hewa iliyotuathiri katika kisiwa chetu.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c). Miongoni mwa kilio cha nchi maskini katika mkutano ule ni kuzitaka nchi za viwanda kupunguza uzalishaji wa madini joto ambayo huchangia sana katika uharibifu wa *ozone layer*.

(a) Mhe. Spika, naomba nieleweshwe kilio kile kiliitikiwa vipi na mataifa ya viwanda.

(b) Kadri tabaka la hewa hili la *ozone layer* linavyoharibika ndivyo dunia inavyoathirika. Wataalamu wanasema kwamba ikiendelea hivi hivi dunia iko hatarini. Je, kwa sasa hali ya dunia ikoje.

(c) Nchi zote duniani ziliwapeleka waandishi wa habari na takwimu zinaonesha kwamba waandishi wa habari 3,500 walihudhuria. Ni kwa nini ujumbe wa Zanzibar haukuchukua mwandishi wa habari ili Wazanzibari wakaelimika.

(d) Wapo wanaoamini kwamba matukio ya karibuni ya nchi ya Haiti ni miongoni mwa athari za hali ya hewa. Je, nini kauli ya SMZ.

**Mhe. Spika:** Mhe. Hija Hassan Hija unakwenda kinyume na kauli yako ya awali. Ulisema swali (a), (b) na (c), imekuwa mpaka (d), sasa hili moja mimi nilipunguze. Moja lilisema kwamba kutafanyika mkutano mwengine *Mexico City*, linajibu swali lako la (a). Mhe. Waziri, jibu maswali matatu yaliyobaki.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunijibia swali la kwanza ambalo tulikwisha kulijibu.

Mhe. Spika, jibu (b) bila shaka kutokana na nilivyoeleza hapa kwa ufupi kwamba Wajumbe wako tutawaletea taarifa kamili iliyotimia, ni warka mkubwa tu ambayo haya yote yatakuwemo.

Lakini pamoja na hayo, ndio maana vikao hivi vikawa vinafanywa mara kwa mara. Ulifanyika mkutano Rome, Italy mara mbili, ukafanyika mkutano Kyoto Japan, umefanyika mkutano wa juzi na utafanyika mkutano mwengine Mexico. Mikutano hii yote inazungumza suala la maharibiko ya hali ya hewa. Moja katika sababu kubwa sana ya joto duniani ni uharibifu huo aliosema Mhe. Mwakilishi *ozone layer,* yaani tabaka la hali ya hewa sehemu ya juu.

Hiyo, inatokana na wenzetu wenye viwanda vikubwa ambao wametajwa sana ni hawa China na Marekani, wao ndio wenye viwanda vikubwa ndio wa mwanzo wanaoharibu hiyo *ozone layer.*

Mhe. Spika, kwa ufupi napenda kuwaambia kwamba *ozone layer* wanasayansi wamesema inaharibika na inaendelea kuharibika kama hawa wenzetu hawatopunguza hii nyuzi joto. Wanasayansi hawakusema kuwa *degree* fulani.

Kwa hivyo, kama alivyosema kwamba njia ya kufanya ni wenzetu kupunguza nyuzi joto ili hali ya joto ipungue na bila shaka *ozone layer* itasita kuharibika. Ikiwa haiendelei kuharibika basi hali ya joto itapungua.

Mhe. Spika, dunia nzima sasa hivi iko katika hali mbaya sana, nafikiri tunafuatilia katika redio na TV. Amesema hapa Mhe. Naibu Waziri kwamba takriban nchi nyingi sana sasa hivi duniani kubwa kubwa zinakumbwa na mafuriko makubwa. Mpaka Ireland kule ambayo haijapata kutokea kwa miaka mingi imetokea, ukienda Thailand, Finland, China, nchi nyingi sana sasa hivi zinakumbwa na mafuriko au baridi kali sana.

Mhe. Spika, juzi tulipokuwa tunarudi Denmark, basi ilikuwa tusiondoke kutokana na hali ya hewa ilivyobadilika. Tuliondoka kule tumefika Hamburg Germany, pale pale halikadhalika hali imekuwa mbaya zaidi hata wenyewe wale wazungu wanasema haijapata kutokea maisha, hawakumbuki. Kwa hivyo, wana vifaa vya kufanyia kazi kuondoa zile barafu saa 24 katika njia za kurukia ndege. Kuna vifaa vya maji ya moto, chumvi, trekta maalumu za kuokoa na kadhalika. Sasa mabadiliko haya ya dunia kwa kweli ni dunia nzima, hakuna pahala pamoja palipokuwa kidogo afadhali.

Swali la kwa nini Zanzibar hatukupeleka mwandishi. Pengine sisi kwa upande wetu kama ni wizara kutokana na hali ya uchumi. Lakini wenzetu wanaohusika na habari sijui wao kwa upande huu hawakuweza kupeleka kwa vipi, lakini nafikiri kwa jumla inatokana na hali yetu ya uchumi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika, kwa upande wa waandishi wa habari lilitolewa tangazo rasmi na *World Meteorological Organization (WMO)* pamoja na waandazi wa hiyo *Copenhagen Conference*, pamoja na Ubalozi wa Denmark uliokuwepo hapa nchini, walitoa tangazo kwa wale waliokuwa na fani ya uandishi wa habari katika fani ya mazingira.

Kwa sababu waandishi wa habari wako wa aina nyingi, wako waandishi wa habari wa kisiasa, waandishi wa habari wa mazingira, waandishi wa habari wa michezo. Wao walitolewa tangazo hilo rasmi kwamba wanaweza kuomba moja kwa moja kupitia Ubalozi wa Denmark pale Dar es Salaam ili kuweza kwenda huko. Kwa hiyo, hilo halikuwa moja kwa moja kwenye mikono ya serikali, ilikuwa ni waandishi wanaweza kuomba moja kwa moja kwa ajili ya kuhudhuria mkutano huo.

**Nam. 68**

**Kudumaa kwa Sekta ya Viwanda Zanzibar**

**Mhe. Ali Abdalla Ali –** Aliuliza:-

Sekta ya Viwanda hapa Zanzibar imedumaa na haikui ipasavyo. Kutokuwepo kwa umeme wa uhakika, ughali wa umeme na kutokuwepo kwa malighafi zinazohitajika kwa uzalishaji, inasemekana kuwa ni miongoni mwa sababu zinazowarudisha nyuma wawekezaji katika sekta hiyo.

(a) Je, Mhe. Waziri, ukweli ukoje kuhusu jambo hilo.

(b) Wizara yako inazishughulikiaje changamoto hizi.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji –** Alijibu:-
Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba kutokuwepo umeme kwa uhakika, ughali wa umeme huo na kutokuwepo kwa malighafi zinazohitajika kwa uzalishaji ni miongoni mwa sababu zinazowarudisha nyuma wawekezaji katika Sekta ya Viwanda kwani bila ya umeme wa uhakika na upatikanaji wa malighafi usioridhisha, shughuli za uzalishaji viwandani huathirika kwa kiwango kikubwa, hivyo kupelekea kupata hasara kwa wawekezaji na taifa kwa jumla.

(b) Mhe. Spika, katika kuzishughulikia changamoto hizo (umeme na uhaba wa malighafi), Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuzizungumza changamoto hizo katika vikao vya Baraza la Biashara la Zanzibar ambavyo vinajumuisha Sekta Binafsi na Sekta ya Umma ili kwa pamoja tuweze kutafuta ufumbuzi.

(ii) Kufanya tafiti za mazao ya kilimo na mazao ya baharini ili yatumike kama malighafi za viwanda vitakavyokuwepo hapa nchini.

(iii) Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kuanzisha matumizi ya nishati mbadala kwa matumizi ya wafanyabiashara wadogo wadogo. Haya tumeweka kama mfano katika Kituo cha Kisakasaka ambapo kunatumika samadi ya ng'ombe kuzalisha umeme. Lakini pia kuna sehemu ambazo tunatumia umeme wa jua na kufunganisha ndani ya viwanda vidogo vidogo kama kuonesha mfano kwa wafanyabiashara wadogo wadogo. Kama ilivyoelezwa juzi na jana katika Sera ya Nishati kwamba serikali kwa ujumla itafanyia kazi suala la nishati mbadala ili pia iweze kutumika kwenye uzalishaji wa viwanda vikubwa.

(iv) Kuhimiza na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kusarifu mazao ya kilimo na bahari ili kuhakikisha kwamba kuna malighafi ya kutosha hapa nchini, au viwanda vilivyopo vitumie malighafi zinazopatikana hapa nchini.

**Mhe. Nassor Ahmed Mazrui:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, viwanda vingi vya Tanzania Bara vinategemea soko lake Zanzibar, lakini kwa bahati mbaya viwanda vingi vya Zanzibar hapo awali vilifungwa kwa kukosa soko Tanzania Bara. Je, Mhe. Waziri, huoni kwamba kuna mkakati maalumu wa kuua Sekta ya Viwanda Zanzibar kwa sababu ya maslahi ya Tanzania Bara.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, ni kweli kwamba viwanda vingi vilivyopo Zanzibar vinategemea soko Tanzania Bara na nje ya Tanzania Bara.

Kwa mfano viwanda vilivyoko *Amani Industrial Park* ambavyo vinazalisha *cassette (audio na video)* lakini pia Kiwanda cha Maplastiki na kiwanda kinacho-*recycle* nguo cha mitumba. Vyote vinategemea soko Tanzania Bara na nje ya Tanzania Bara na hasa *East Africa* na *Central Africa*.

Ni kweli pia kwamba kulikuwa na vikwazo wakati wa kupitisha mizigo hiyo kwenda nje au kuingia ndani ya Tanzania Bara. Lakini hili tumelifanyia kazi na kama nilivyojibu jana kwa kiasi kikubwa malalamiko yamepungua. Kwa hiyo, tutaendelea kulifanyia kazi na kuhakikisha kwamba bidhaa zinazozalishwa Zanzibar zinakwenda kwenye soko lililotarajiwa.

**Nam. 22**

**Barabara ya Kidimni – Ubago**

**Mhe. Haji Mkema Haji –** Aliuliza:-

(a) Kwa nini barabara ya Kidimni hadi Ubago ambayo ilijengwa tangu 1968 haitunzwi kwa kutiwa viraka au kutengenezwa misingi yake ya maji.

(b) Kutokana na umri mrefu barabara hiyo imechakaa sana na kuwa na mashimo yenye hatari. Je, serikali itachukua hatua gani za dharura kuihami barabara hiyo.

(c) Kwa sababu barabara hii ni muhimu sana kwa wakulima na taasisi za serikali. Je, unaonaje ikafanyiwa *feasibility study* na kutafutiwa ufadhili ili ijengwe upya.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi –** Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Nakubali kuwa barabara ya Kidimni hadi Ubago imejengwa tangu mwaka 1968 kwa utaalamu wa kizamani wa kupanga mawe. Kutokana na hali hiyo barabara si rahisi kuweza kuiziba viraka. Wizara yangu inakusudia kuijenga barabara hiyo katika mwaka wa fedha 2010/2011.

**Nam. 10**

**Matengenezo ya Uwanja wa Mao Tse Tung**

**Mhe. Ali Suleiman Ali –** Aliuliza:-

Kuimarisha viwanja vya michezo nchini ni hatua moja wapo ya kuimarisha michezo nchini.

Mhe. Waziri, lini Uwanja wa Mpira wa Miguu wa Mao TseTung utafanyiwa matengenezo makubwa ili kuuweka katika hali nzuri kimchezo na kunyanyua haiba yake na haiba ya mji wetu wa Zanzibar.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo –** Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa kuimarisha viwanja vya michezo ni hatua moja wapo muhimu sana ya kuimarisha michezo hapa nchini kwetu.

Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara yetu ya Habari, Utamaduni na Michezo, imekuwa ikichukua hatua za makusudi katika kuhakikisha kuwa viwanja vyetu vya michezo vinaimarishwa kila hali inaporuhusu.

Mhe. Spika, hivi sasa kiwanja cha Amaan kinafanyiwa matengenezo makubwa na muda si mrefu kiwanja cha Gombani nacho kitafanyiwa matengenezo mengine makubwa kama hayo.

Mhe. Spika, ni lengo la serikali kuona kuwa kiwanja vya Mao Tse Tung nacho kinafanyiwa matengenezo makubwa katika ile nia yetu ya kuimarisha viwanja vya michezo nchini. Hvi sasa tumo katika mazungumzo kupitia Afisi ya Mhe. Waziri mwenyewe na kampuni moja wapo ya kibiashara ili kufunga nao mkataba kwa ajili ya kiwanja hicho.

Aidha, kuna mpango wa kutenga viwanja viwili katika kila mkoa ili kuvisajili na kuvitengeneza viwe na sura mpya kwa kila mkoa kwa Unguja na Pemba. Pia, kushirikisha Sekta Binafsi katika kuvikuza na kuviendeleza kibiashara.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Habari, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri katika nchi za wenzetu kama Uganda kiwanja cha Nakivubo kiko

katikati ya mji ambacho ni kidogo kama cha Mao Tse Tung. Lakini kutokana na kiwanja kile cha historia kilivyowekwa ni kiwanja kinachochezeka michezo ya kimataifa bila ya tatizo. Kwa kuwa swali langu nilimuuliza Mhe. Waziri uwanja wa Mao Tse Tung ni muhimu na pale ulipo una historia kubwa ya Kiongozi wa China Mao Tse Tunge.

Je, angalau ilitokea siku moja au ana mpango wa kumualika Balozi wa China kuja kutembelea uwanja ule hasa kwa kuwa tuna mkataba mzuri wa kutujengea uwanja mpya hivi sasa kuona lile jina lao liweke ubora zaidi, au wanaweza kulifadhili bila ya kumuomba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika, wazo hilo tutalichukua na tutalifanyia kazi.

**Nam. 62**

**Ada ya Uwekezaji katika Elimu**

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Ali Abdalla Ali) –** Aliuliza:-

Serikali imetoa fursa kwa mwenye uwezo wa kuwekeza katika elimu. Fursa hiyo imetumiwa na wazalendo pamoja na wageni. Shule zimefunguliwa katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba, kuanzia elimu ya msingi, sekondari na vyuo vikuu.

(a) Je, Mhe. Waziri unajua kwamba shule hizo zinapitana kwa wingi wa majengo na idadi ya wanafunzi lakini wote wanatozwa ada kiwango kimoja.

(b) Kwa nini shule za binafsi ziruhusiwe kutumia mitaala tofauti na ile inayotumiwa na shule za serikali.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali –** Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijamjibu swali lake Mhe. Mwakilishi, naomba nitoe taarifa kwamba Mhe. Waziri sasa hivi amekwenda kutoa taarifa ya matokeo ya mitihani na napenda niwapongeze wananchi, viongozi, wanafunzi na walimu kwa kuyafanya matokeo ya mwaka huu kuwa mazuri zaidi. Tunatarajia kutoa matokeo hayo mwisho wa wiki hii.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, skuli za binafsi hazitozi ada za viwango tofauti bali zinatoa ada za viwango vya aina moja.

(b) Mhe. Spika, skuli zote binafsi zinapaswa kufuata mihutasari au mitaala inayopitishwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali au Serikali. Hata hivyo, skuli binafsi zinazotaka kuongeza baadhi ya mada au masomo ambayo hayafundishwi katika skuli za serikali, inalazimika ziombe kibali kutoka Wizarani.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante Mhe. Spika, kwa faida ya wananchi wetu. Hivi sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania suala la elimu kuanzia kidato cha kwanza, kidato cha pili na kidato cha sita, wamefutiwa kulipa ada katika mitihani yao ya kitaifa yote. Je, kwa kuwa fursa hiyo na mitihani hiyo ni moja kwa Tanzania nzima, sisi tumefaidika vipi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, sisi hapa Zanzibar masomo ya darasa la kumi na mbili mpaka sasa hivi serikali inafidia ada hizo za mitihani, isipokuwa tunalipia masomo ya darasa la kumi na nne. Hata hivyo, wizara inalifikiria wazo hilo la kufuta au kuondoa hizo ada kama wenzetu walivyofanya, ni ada ya mitihani.

## HOJA ZA SERIKALI

### Ripoti ya Uchunguzi wa Ajali ya Meli ya LCT Fatih

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu nisome mapendekezo ya wizara baada ya kupata ripoti ya bodi ya uchunguzi wa meli ya LCT Fatih.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kusoma, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba bodi ilifanya kazi nzuri, ilichukua muda kidogo lakini matokeo yake yalikuwa mazuri. Nafikiri kwa wale watakaotaka kukisoma kitabu hiki, basi tayari kipo afisini kwa Mhe. Spika.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba nianze kusoma Ripoti ya Uchunguzi wa Kuzama Meli ya MV Fatih katika Bandari ya Malindi Zanzibar.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, naomba kutoa taarifa kwamba siku ya Ijumaa tarehe 29 Mei, 2009 saa 4:00 za usiku, meli ya LCT Fatih ikiwa na abiria wanaosemekana 25 walioorodheshwa katika orodha maalumu ya abiria, *passengers list* na tani 55 ya mizigo ziliorodheshwa. Chombo hicho kilipinduka wakati kikifunga gati katika Bandari ya Malindi iliopo Mjini Zanzibar ikitokea Dar es Salaam.

Katika ajali hiyo jumla ya abiria sita walifariki dunia na watu 36 waliokolewa. Maiti watatu waliopolewa siku ya kwanza ya tukio, kwenye majira ya saa 9:00 za usiku na maiti watatu wengine wakiwemo watoto wawili na mtu mzima mmoja waliopolewa siku ya pili yake.

Shughuli za uokozi wa mali na abiria pamoja na kuirejesha meli katika hali ya kawaida, ilifanywa na Shirika la Bandari kwa kusaidiana na Vikosi vya Ulinzi na Uokozi vya Zanzibar na vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, vikishirikiana na taasisi mbali mbali hapa Zanzibar na ilichukua jumla ya siku sita kuanzia siku ya tukio hadi tarehe 5 Juni, 2009, ndipo kazi ilipokamilika.

Kwa mujibu wa sheria nambari 5 ya mwaka 2006 inayoelekeza namna ya kusimamia na kuendesha shughuli za baharini Zanzibar. Mimi nikiwa Waziri wa Nchi Afisi ya Rais ninayeshughulikia mambo ya Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, niliunda bodi ya watu sita kufanya uchunguzi wa ajali hiyo. Bodi hiyo iliongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, akisaidiwa na Wajumbe wake.

Mhe. Spika, bodi hiyo kama nilivyosema iliongozwa na:

1. Mhe. Jaji wa Mahakama Kuu Zanzibar, Omar O. Makungu Mwenyekiti, akiwa na Wajumbe wake
2. Captain Al Hajj Masoud Sururu
3. Captain William Mlesa
4. Captain Moh'd M. Juma
5. Ndg. Abdalla H. Kombo
6. Engineer Abdi O. Maalim

Mhe. Spika, bodi hii ilifanya kazi kwa kusaidiwa na makatibu wawili,

Ndg. Khalfan S. Omar - Katibu na
Ndg. Hassan A. Haji - Msaidizi Katibu kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar.

Mhe. Spika, bodi ilifanya kazi hiyo kwa muda wa mwezi mmoja na nusu, kuanzia tarehe 11 Juni, 2009 ilipozinduliwa. Katika kipindi hicho ilikusanya

taarifa na maelezo muhimu kwa kupitia nyaraka mbali mbali na kusaili mabaharia, abiria na watendaji wa taasisi za serikali na watu binafsi mbali mbali kwa Zanzibar na Tanzania Bara. Kwa ujumla bodi iliwahoji kiasi ya watu 75.

Katika uchunguzi wake, bodi imeridhika na mambo ambayo yalisababisha meli hiyo kuzama au kupinduka ni haya yafuatayo:-

a) Meli iliingiza maji kupitia kwenye mlango wa mbele *ramp* na kwenye matundu katika sehemu ya chini ya meli *bottom plate*.

b) Meli ilikuwa haina mfumo wa kuingiza na kutoa maji *ballast water pump* katika matangi ya farumu *ballast tanks* kutokana na muundo yaliyofanywa huko nyuma nchini Madagascar. Hali hii ilisababisha maji yaliyoingia kama nilivyoeleza katika kipengele cha kwanza juu, kushindwa kutolewa wakati wa dharura.

c) Uzembe wa Nahodha wa kutotoa taarifa ya hali ya hatari na kuomba msaada kwa vyombo vinavyohusika, akijua kwamba meli yake imepakia abiria na mizigo na iko katika hatari ya kuzama.

d) Uzembe na Nahodha wa kutotimiza wajibu wake wa kuokoa maisha ya watu, kwa kushindwa kuipeleka meli sehemu ya mchanga, huku akijua kwamba hali ya hatari waliyonayo katika meli inaweza kutokea ajali, kwa sababu meli ilianza kupata matatizo tangu Pungume.

Mbali ya masuala hayo, bodi ilione kuwa kuna masuala mbali mbali, ambayo hayakuwa ni miongoni mwa sababu za ajali, lakini yanahitaji kuangaliwa katika kuimarisha usalma wa vyombo baharini. Masuala hayo yanaelezwa katika sehemu ya tano ya ripoti ya uchunguzi. Baadhi ya mambo hayo ni haya yafuatayo:-

i Ukosefu wa elimu na uzoefu wa kutosha kwa mabaharia juu ya kutoa msaada kwa abiria wakati wa ajali.

ii Kukosekana kwa usimamizi wa uorodheshaji wa abiria na mizigo katika bandari ya Dar es Salaam na Zanzibar.

iii Ukosefu wa vifaa vya udhibiti wa mizigo ndani ya meli.

iv Utaalamu mdogo kwa baadhi ya wafanyakazi na ukosefu wa vifaa muhimu vya kutendea kazi katika kitengo cha usajili wa meli Zanzibar.

Kufuatia ripoti hii ambayo imetoa uchambuzi wa kina juu ya ajali hii, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, inatoa mapendekezo mbali mbali yanayoelekeza hatua ambazo imepanga kuzitekeleza mara moja juu ya ajali hiyo na katika kuboresha usalama wa vyombo vya baharini Zanzibar. Mapendekezo hayo yamezingatia udhibiti wa usafiri wa baharini katika maeneo yafuatayo:-

a) Hatua za kisheria za kuchukuliwa kwa wahusika,

b) Hatua za kinidhamu za kuchukuliwa kwa wahusika,

c) Malipo ya fidia kwa waathirika wa meli ya LCT Fatih,

d) Marekebisho ya sheria na kanuni,

e) Uimarishaji wa taasisi zinazohusika,

f) Utekelezaji na usimamizi wa sheria na kanuni.

(a) Mhe. Spika, hatua za kisheria kwa wahusika. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi inapendekeza kuwa wahusika wafuatao wachukuliwe hatua za kisheria ikiwemo kushtakiwa kwa mujibu wa sheria.

Nahodha wa meli kwa kusababisha ajali na kupoteza mali na watu.

(b) Hatua za kinidhamu kwa wahusika. Wizara inachukua hatua zifuatazo za kinidhamu
kwa wahusika wafuatao:-

1. Nahodha atasimamishwa cheti chake kwa kipindi muafaka kwa;

- Kushindwa kutoa maamuzi sahihi ya kiutendaji ya kuepusha ajali kwa mujibu wa taaluma yake.

- Kushindwa kutoa taarifa ya hali ya hatari kwa vyombo husika wakati meli ilipokuwa ikiingiza maji,

- Kushindwa kutoa msaada kwa abiria wakati wa ajali,

- Kutoa taarifa za uongo mbele ya bodi.

2. Mabaharia sita wa meli hiyo ya MV Fatih waliosailiwa na bodi, vyeti vyao vitasimamishwa kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa kutokutekeleza wajibu wao wa uokozi wa abiria na kutoa maelezo ya uongo mbele ya bodi.

3. Kampuni ya ukaguzi wa meli iliyoikagua meli ya MV Fatih itachukuliwa hatua za kutozwa faini kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

4. Watendaji wa Afisi ya Mrajis waliohusika kutoa vyeti batili kwa meli hiyo kinyume na sheria watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria za kazi.

(c) Malipo ya fidia kwa waathirika wa Meli ya MV Fatih. Kwa mujibu wa sheria nambari 5 ya mwaka 2006, wizara inamtaka mmiliki wa meli hiyo alipe fidia kwa maelekezo ya sheria, jamaa wa watu waliofariki, abiria na wale waliopoteza mali zao katika ajali hiyo. Hata hivyo, sheria inawatambua wale wote ambao waliingia wakiwa na tiketi halali kama abiria halali na ndio watakaopaswa kulipwa fidia.

(d) Uimarishaji wa taasisi. Afisi ya Mrajisi wa Meli Zanzibar.

(i) Mhe. Spika, Wizara itachukua hatua za makusudi za kuimarisha Afisi ya Mrajis wa meli ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ili kuweza kufikia hayo, wizara itayatekeleza yafuatayo:-

- Afisi ya Mrajis wa Meli itapatiwa wataalamu wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha katika fani ya ubaharia na utawala.

- Afisi ya Mrajis wa Meli, vifaa na zana za kutosha za kufanyia kazi, vikiwemo vifaa vya kisasa vya ukaguzi kila hali ya fedha itakaporuhusu.

- Wafanyakazi watapatiwa mafunzo kila baada ya muda ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia za meli.

- Utaandaliwa mfumo mahususi wa utumishi utakaowawezesha wakaguzi kulipwa mishahara stahiki pamoja na marupurupu mengine, ili kuepusha uwezekano wa kupokea hongo kutoka kwa wamiliki wa meli.

(ii) Mhe. Spika, wizara itahakikisha kuwa Afisi ya Mrajis wa Meli itachukua hatua zifuatazo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji wake;

- Itahakikisha kwamba usajili wa meli unafuata taratibu zote husika kwa mujibu wa sheria ya usafiri baharini, sheria nambari 5 ya mwaka 2006 pamoja na kanuni zake;

- Pia, katika usajili wa vyombo, itaandaa utaratibu wa kuweka nakala za vyeti na nyaraka muhimu za meli husika, zikiwemo kitabu cha *stability data book, past survey report, ship plans* na nyenginezo;

- Aidha, kwa kushirikiana na kampuni za meli itahakikisha kuwa mabaharia wanaelewa wajibu wao wakati wa ajali na uokozi ili waweze kushiriki ipasavyo katika kuokoa watu na mali zao wakati wa ajali;

- Itaandaa utaratibu wa kuwaelimisha wafanyabiashara wenye kuendesha biashara ya meli kwa kuzingatia umuhimu wa mambo yafuatayo:-

    1) Kununua meli zilizo salama;

    2) Kuendesha biashara ya meli kwa kufuata sheria na kanuni za kitaifa na kimataifa;

    3) Kuzifanyia matengenezo meli zao kwa wakati unaofaa;

    4) Kuwaajiri wataalamu wa meli ili kusimamia shughuli za meli na kuwapa mamlaka kamili ya kuziendesha kulingana na sheria na taratibu zilizopo.

v) Aidha, itaziagiza kampuni za meli kutoa hati za mizigo yaani *cargo consignment note* kwa watu wanaopakia mizigo yao katika meli ili wawezeshe wenye mizigo kuwa na kumbukumbu za mizigo waliopakia katika meli zao;

vi) Itachukua hatua za kufuatilia sifa za mabaharia melini, ili kuhakikisha kwamba mabaharia wanafanyakazi kulingana na sifa na ujuzi, kama ilivyoelezwa katika sheria na kanuni zilizopo;

vii) Pia, itaandaa na kusimamia mazoezi ya mabaharia kila kipindi kwa meli zote zilizosajiliwa Zanzibar;

- Mhe. Spika, kwa upande wa Shirika la Bandari. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi itahakikisha kwamba Shirika la Bandari linanunua vifaa vya uokozi baharini ili kukabiliana na ajali zinazotokea katika bandari zake;

- Wizara itahakikisha kuwa Shirika la Bandari linaweka taa katika eneo lote la bandari;

- Wizara itahakikisha kuwa Shirika la Bandari linaandaa mpango wa dharura wa kupambana na ajali ili kuweza kujenga uwezo wa kukabiliana na ajali zinazotokea katika eneo lake la bandari;

(e) Marekebisho ya Sheria na Kanuni.

(i) Mhe. Spika, wizara yangu inakusudia kufanya marekebisho ya sheria nambari 5 ya mwaka 2006 katika maeneo yafuatayo:-

- Kuingiza kifungu cha ukomo wa umri ambao meli ikizidi haitosajiliwa katika *register* ya Zanzibar;

- Kitaingizwa kifungu kitakachokataza wenye meli kufanya mabadiliko au matengenezo ya meli bila kusimamiwa na mkaguzi anayetambulika pamoja na Mrajis wa meli, mabadiliko hayo yatalazimika kupata idhini ya waziri anayehusika au anayeshughulikia na mambo ya usafiri wa baharini;

(ii) Kufuatia ajali hii na uchunguzi uliofanywa na wataalamu wetu, wizara yangu inakusudia kurekebisha kanuni za usajili na leseni za vyombo baharini za mwaka 2007 kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- Kuingiza sharti kwa waombaji wa usajili wa muda wa meli zilizotumika yaani *second hand*, kupeleka mkaguzi kwenda kuzikagua au kutafuta mkaguzi yeyote anayetambulika kuikagua na kuleta ripoti yake kabla usajili wa muda kutolewa;

- Kuingiza sharti la utoaji wa hati ya usalama wa mizigo yaani *cargo safety certificate*, kama ilivyotajwa kwenye sheria;

(iii) Wizara imeteua kamati maalumu ya kumalizia utayarishaji wa kanuni zote za sheria nambari 5 ya mwaka 2006, ambazo bado hazijatayarishwa ili kurahisisha utekelezaji na usimamizi bora wa sheria yenyewe.

(iv) Kamati hiyo maalumu pia itaandaa utaratibu au kanuni za kuzitaka kampuni za meli, kutokupewa leseni za kuendesha biashara hiyo kabla ya kuanza biashara. Utoaji wa leseni hizo uwe na masharti mbali mbali likiwemo sharti la kampuni kuwa na watu wenye ujuzi na uzoefu wa shughuli za uendeshaji wa meli.

(v) Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, imewasiliana na watendaji wa pande zote mbili za Muungano na kuwataka watekeleze sheria zote mbili kikamilifu bila kujali sheria inatoka upande gani wa Muungano, yaani SUMATRA na Mrajis wa Meli;

(f) Mhe. Spika, Kuhusu Utekelezaji wa Usimamizi wa Sheria.

(i) Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar imo katika hatua za mwisho za kuanzisha mamlaka ya usafiri baharini chini ya sheria nambari 3 ya mwaka 2009. Wizara itahakikisha kuwa mamlaka hii inaanzishwa kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

(ii) Wizara yangu itahakikisha kuwa Shirika la Bandari Zanzibar, Mamlaka ya Udhibiti wa Bandari Dar es Salaam, Afisi ya Mrajis wa Meli Zanzibar na SUMATRA Dar es Salaam na Kampuni za Meli, zinaandaa mkakati na mipango ya kusimamia uingiaji na uteremshaji wa abiria na mizigo melini, utakaohakikisha kuwa kuna uwiano wa takwimu miongoni mwa taasisi husika. Kila taasisi iwe na taratibu ambazo kila mmoja atajua kuwa abiria ni wangapi na mizigo ni mingapi.

(iii) Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu ya Serikali ya Muungano wa Tanzania, itahakikisha kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri nchi kavu SUMATRA, kwa kushirikiana na Afisi ya Mrajis wa Meli Zanzibar, wanasimamia utekelezaji wa kujaza fomu ya usalama, yaani *safety form*, kwa manahodha wa meli zinazoingia na kutoka bandarini ili kuhakikisha kuwa usalama wakati wa kuingia na kutoka bandarini unakuwepo.

(iv) Hivi sasa wizara imetoa agizo kwa makampuni yote yanayouza tiketi za abiria wa usafiri wa baharini Zanzibar, kuhakikisha kwamba abiria wote wananunua tiketi hizo kwa kutoa vitambulisho vyao kabla ya kuuziwa tiketi hizo.

(v) Wizara itahakikisha kwamba Afisi ya Mrajis itafanya taratibu za kuhakikisha kuwa *safety management system,* inayofanana na *ISM code* inatekelezwa na makampuni ya meli yanayopewa leseni ya kuendesha meli hapa Zanzibar.

(vi) Wizara yangu imeshaanza zoezi la kuhakikisha kuwa meli zote zilizosajiliwa Bandari ya Zanzibar kuchukua abiria, zinakaguliwa upya kwa kufuata taratibu za kisheria na kanuni za kimataifa.

**Hitimisho**

Mhe. Spika, ajali ya kupinduka meli ya MV Fatih katika Bandari ya Zanzibar tarehe 29/5/2009, ni tukio lililoleta msiba, huzuni na majonzi kwa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla. Katika ajali hiyo jumla ya watu 6 wamepoteza maisha yao na mali kadhaa zimeharibika na kupotea.

Tumejifunza mengi miongoni mwetu, lakini kubwa ni kuwa Zanzibar kama nchi ya bahari shughuli za kila siku za wananchi zinategemea usafiri wa baharini. Hii ina maanisha kwamba juhudi za makusudi zinahitajika kuimarisha usalama wa usafiri wa baharini ili kuepuka majanga mengine kama ya LCT Fatih kutokea.

Wananchi nao wanao wajibu wa kuwa na tahadhari na kufuata maagizo na taratibu za sheria za usafiri wa baharini, ili kuepuka ajali hizo zinazoweza kuepukika. Serikali kwa upande wake itahakikisha kuwa sheria na taratibu za usalama baharini zinatekelezwa ipasavyo.

Bila shaka ni kwa mantiki hiyo ndio maana serikali ikaunda bodi ya uchunguzi wa ajali hii, ili iweze kueleza umma wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla, sababu na mazingira yaliyosababisha ajali hiyo na pia kutoa ushauri ambao utasaidia kuepusha ajali nyengine kama hizo zinazoweza kutokea katika siku za baadae.

Wizara yangu inaamini kuwa mapendekezo yaliomo katika ripoti ya uchunguzi wa kuzama kwa meli ya MV Fatih, yatasaidia sana kupunguza idadi za ajali za baharini Zanzibar na kwa zile zitakazotokea kwa mazingira mbali mbali kama hali ya hewa, Madhara yake yatakuwa ni madogo sana. Hivyo, wizara itahakikisha kuwa mapendekezo yatafanyiwa kazi ipasavyo na yatakuwa msingi wa juhudi itakayoweka mwelekeo na utamaduni mpya wa nchi yetu katika kushughulikia usalama wa vyombo vya baharini.

Wizara inaelewa kuwa mapendekezo haya ni changamoto kubwa kwa taifa, kwani utekelezaji wake unahitaji fedha na kwa wakati huu ambapo serikali inakabiliwa na ufinyu wa bajeti katika utekelezaji wa vipaumbele vya mpango wa kupunguza umaskini. Hata hivyo, ni mategemeo ya wizara yangu kuwa serikali wenye meli na wananchi wote kwa ujumla tutatumia busara, hekima na ujasiri kuona kuwa mapendekezo hayo yanatekelezwa ili kunusuru maisha ya watu na mali ambazo ni rasilimali ya nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe hiyo ni taarifa ya ripoti ambayo imeletwa kuhusiana na ajali ambayo ilitokea kwenye mwezi wa Mei mwaka jana. Nafikiri mtakuwa mmeona kuwa jambo hili limekuwa na mambo mengi ndani yake. Kwa kweli umuhimu wa kuja taarifa hii ulikuwepo, isipokuwa tu ilikuwa imekawia, sijui kwa sababu ya uzito wa jambo lenyewe au vipi, lakini hatimae umuhimu wa kutoa taarifa hii kama vile ambavyo Mhe. Waziri alikubali mapema wakati wa mkutano wa bajeti uliopita, umuhimu huu kumbe upo mkubwa.

Sasa taratibu za taarifa kama hii huwa haijadiliwi, isipokuwa tu baada ya taarifa ya Mhe. Waziri huwa tunamkaribisha Mhe. Waziri Kivuli, ili kutoa maoni ya upande wa Kambi ya Upinzani juu ya jambo hili na juu ya ripoti hii. Sasa nimkaribishe basi Waziri Kivuli wa Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi, Mhe. Omar Ali Shehe, ili aje atowe maoni ya Kambi ya Upinzani.

**Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, sina budi nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia afya na uwezo na leo hii tukaweza kukutana hapa. Aidha, nikushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ili nieleze machache juu ya ripoti inayohusiana na ajali ya

Meli ya MV Fatih iliyotokea usiku ya Ijumaa ya tarehe 29 Me, 2009 wakati ilipokuwa ikifunga gati katika Bandari ya Malindi ikitokea Dar es Salaam. Tukio ambalo lilipoteza maisha ya wenzetu na mali zao nyingi kupotea na kuharibika.

Mhe. Spika, tunakumbuka kuwa tukio la kuzama kwa meli ya MV Fatih katika Bandari ya Malindi lilivuta na kuibua hisia za wananchi waliowengi ndani na nje ya nchi yetu kwa sura mbili kuu.

1. Hali ya kutokea kwa ajali za baharini mara kwa mara kati ya visiwa vyetu na mwambao wa Dar es Salaam, Tanga na Mombasa;

2. Uwezo wa mamlaka zinazohusika katika kukabiliana na maafa wakati yanapotokea.

Mhe. Spika, tukio la kuzama kwa meli hiyo katika Bandari ya Malindi ambapo ilichukua zaidi ya siku sita katika harakati za uokozi ni kielelezo cha unyeti wa tatizo la usalama katika usafiri wa bahari hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi anayeshughulikia Mawasiliano na Uchukuzi, kwa utekelezaji wa ahadi yake aliyoitoa mbele ya Baraza lako tukufu la kuunda bodi iliyopewa jukumu la kuchunguza tukio la kuzama kwa meli hiyo. Aidha naomba pia niitumie fursa hii kuipongeza bodi iliyoundwa kwa kazi kubwa na nzuri walioifanya licha ya kukabiliwa na vikwazo kadhaa kama vile muda, bajeti na ukosefu wa mashirikiano kwa baadhi ya wahusika.

Bodi iliyoundwa imeainisha kasoro mbali mbali zilizochangia kubiruka na kuzama kwa meli hiyo. Kasoro ya ukiukwaji wa sheria na kanuni za usafirishaji, taratibu za usajili na kadhalika. Serikali nayo kwa upande wake imeeleza hatua mbali mbali itakayozichukua kwa watakaobainika kuzembea na kukiuka kwa taratibu, kurekebisha mapungufu yaliyomo kwenye sheria na kanuni za usajili na usafirishaji wa baharini.

Mhe. Spika, baada ya tukio la kuzama kwa meli hiyo, kuna matokeo kadhaa yaliyotokea na ambayo yalizihusu meli zetu. Ni juzi tu tarehe 24/01/2010, meli ya Sea Guly iliyokuwa na abiria zaidi ya 300, iliyokuwa ikitokea kwenye Bandari ya Dar es Salaam ilizimika zaidi ya masaa 3 na kuzusha tafrani kubwa kwa abiria hao ndani ya chombo hicho. Naiomba serikali iwe makini sana katika kutekeleza yale yote yaliyoelezwa kwenye ripoti hiyo na mengine mengi ambayo hayakugunduliwa kwa vile hayakujitokeza kwenye mapungufu yaliyosababisha chanzo cha kuzama kwa meli ya MV Fatih.

Mhe. Spika, naamini kwamba usalama wa sekta ya usafiri wa baharini bado inakabiliwa na changamoto kubwa. Ripoti hii inahusu uchunguzi uliohusu tokeo moja tu, kwa wakati ambapo kuna matokeo kadhaa yaliyopoteza maisha na mali kadhaa kwa nyakati kadhaa na sehemu kadhaa. Laitani kama kila tokeo lingeundiwa bodi, basi hapana shaka ripoti zingekuwa ni nyingi, mapungufu yangekuwa ni mengi na kwa muhtadha huo huo na serikali nayo kwa upande wake ingekuwa na kibarua kizito katika kujiweka sawa katika kukabiliana na maafa yatokanayo na sekta ya usafiri wa baharini.

Serikali haina budi kuanzisha utamaduni wa kufanya uchunguzi ili kubaini mapungufu katika sekta nyengine za usafiri kama vile anga na nchi kavu ili kuepusha maafa kabla ya kutokea.

Mhe. Spika, pamoja na mapungufu yaliyomo kwenye sheria na kanuni, matatizo ya kiufundi na kimuundo, kukiukwa kwa taratibu zile za kiusajili na kihuduma kwa abiria, uzembe katika usimamizi na utawala, uendeshaji wa vyombo na makampuni yanayomiliki vyombo vya usafiri na kwa upande mwengine wananchi nao wanapaswa wazingatie sana usalama kwa kuepuka kutumia vyombo vya kubahatisha.

Mhe. Spika, suala hii ni gumu lakini ninaamini kuwa iwapo serikali itaandaa utaratibu utakaoelimisha wananchi kutambua tofauti kati ya vyombo salama na visivyo salama, hii inaweza ikawafanya wananchi wakawa ni sehemu ya walinzi na wasimamizi wa sheria na kanuni zetu kwa vile wao ni wadau wakubwa wa usafiri huu.

Mhe. Spika, naomba nimalize kwa kurudia kuipongeza serikali, kupitia kwa Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi kwa hatua hii, huku kambi yangu ikiamini kuwa mapendekezo yaliyotolewa na bodi, nyongeza ya mapendekezo yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani kupitia kwa msemaji wake na mapendekezo yatakayotolewa na Wajumbe wa Baraza hili, yatazingatiwa na kuchukuliwa hatua madhubuti na serikali, ili wananchi wetu waendelee kufurahia maisha yao na mali zao katika harakati za kwenda huku na huko ndani na nje ya visiwa vyetu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha *(Makofi).*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mhe. Omar Ali Shehe. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, serikali imekuwa na maoni kama ilivyotoa ripoti hiyo, pengine imeanza kutekeleza au imetaka itekeleze. Lakini kabla haijakamilisha kufanya hiyo kazi, pengine Wajumbe mtakuwa na maswali mawili au matatu ili kujazia pale ambapo mnaona pengine lipo, ili serikali ipate nguvu ya kutekeleza yale yaliyotajwa kwenye ripoti hii.

Tayari nilikuwa nina jina la Mhe. Zahra Ali Hamad na baada ya hapo nitamwita Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu.

**Mhe. Zahra Ali Hamad:** Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuweza kuuliza swali katika ripoti hii ambayo ni muhimu. Mhe. Spika, naomba unipe fursa nimshukuru Mhe. Waziri, japokuwa kachelewa, lakini katuletea ripoti hii ambayo naamini imekidhi haja na hii bodi imefanya kazi kama ambayo tulitarajia ifanye kazi.

Mhe. Spika, nataka nimuulize Mhe. Waziri, sijui atakubaliana na mimi kuwa mabaharia wetu wengi wana vyeti *fake* na wizara itachukua hatua gani ili kuhakiki vyeti hivi upya.

Mhe. Spika, swali langu la pili, naomba nimuulize Mhe. Waziri kutokana na ripoti hii ilivyojionesha, mmiliki wa meli hii alikuwa na taarifa toka mwanzo kuwa meli yake haiwezi kufanya kazi ikiwa haijafanyiwa matengenezo makubwa tangu alipokwenda kuinunua kule Madagascar.

Hata yule nahodha aliyekwendanaye alimshauri kuwa meli hii aifanyie matengenezo makubwa. Lakini ikaonekana mmiliki wa meli hii kwa sababu moja au nyengine aliona hizi dola alfu saba za Kimarekani ni nyingi sana.Kwa hivyo, ikawa hakuthamini yale maisha ya watu na mali zao. Haoni kama hii adhabu ambayo wameifikiria wizara bado ni ndogo.

Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu:** Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii. Mimi nimesimama kama Ramadhan Nyonje Pandu na sikusimama kama Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Spika, kwanza nataka kuuliza, hizi kanuni zetu katika hoja kama hii mwisho maswali mangapi? Kwa sababu nina maswali kumi nimekusudia kuyauliza. Sasa iko wazi.

**Mhe. Spika:** Spika atazingatia.

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu:** Ahsante, nakushukuru sana na naishukuru serikali nasema hatimaye imetekeleza azma yake ya kuleta taarifa hii, lakini inanisikitisha Mhe. Spika, pale kuona serikali iliyo makini mpaka inasukumwa kutekeleza wajibu wake wa kazi. Ni dhahiri ripoti hii isingekuwa hoja binafsi iliyotaka kuletwa kwenye Baraza hili basi nina hakika isingeletwa.

Mhe. Spika, swali la kwanza nataka kuuliza kwamba, serikali ilipotangaza kuunda tume ya kuchunguza ajali hii tangu tarehe 11/06/2009 mpaka ripoti hii inatolewa karibu ni miezi minane, umekuwa ni muda mrefu sana. Nini sababu ya serikali kuchelewa kuleta ripoti hii ambayo ilimalizika tarehe 11/06/2009.

Pili, wizara imependekeza hatua za kisheria na za kinidhamu zichukuliwe kwa watu wanaohusika. Wizara hii imependekeza hatua hizo zichukuliwe na nani? Kwa sababu ripoti inasema wizara imependekeza hatua za kinidhamu zichukuliwe, nani anayehusika kuchukua hatua hizo za kinidhamu.

Tatu, miongoni mwa hatua za kinidhamu zilizopendekezwa kuchukuliwa kwa wahusika ni pamoja na nahodha kusimamishwa cheti kwa kipindi muwafaka, neno 'kwa kipindi muwafaka' katika ripoti hii lina maana gani? Muwafaka mtapokubaliana au muwafaka maana yake nini katika utekelezaji huo.

Hapa hatuoni kuwa serikali haikuwa wazi kwa kusema kuwa kwa wakati muwafaka, si ingekuwa vizuri basi wakataja kipindi mahsusi kama cha mwaka mmoja, miaka mitano, mwezi au kunyang'anywa leseni moja kwa moja? naona hapo kidogo suala la neno muwafaka serikali kama imeficha namna.

Mhe. Spika, la nne kosa la namna hii la kuzama kwa meli kwa uzembe na kusababisha vifo linachukuliwa ni kosa la kuua. Je, hili ni kosa la kuua bila ya kukusudia au ni kosa la kuua kuwa ndio umeua? Ikithibitika ni kosa la kuua bila ya kukusudia ambalo limesababishwa na uzembe kwa kuendesha meli yenye matundu na kuvujisha maji ndani yake huo ni uzembe. Je, likithibitika kosa la namna hiyo hatua gani za kisheria zitazochukuliwa dhidi ya mhusika aliyetenda kosa hili.

Mhe. Spika, jengine meli hiyo kuna taarifa katika ripoti hii inasemekana imeundwa kwenye mwaka 1979, lakini taarifa nyengine zinasema imeundwa mwaka 1964, kiasi cha kwamba miaka 44 sasa hivi meli hiyo inafanya kazi. Ni muda gani maalum uliowekwa kufanya kazi kwa meli hizi? Miaka 44 inaruhusiwa kuendelea kufanya kazi au ni sababu zipi ambazo ziliendelea kuruhusiwa meli hii kufanya kazi wakati ikionekana kuwa muda huo umekuwa ni mkubwa sana kwa meli hiyo kufanya kazi.

Pengine Mhe. Spika, kwa sababu na wenzangu wanataka kuuliza basi yaliyobakia wengine wananambia nisiyamalize yote nawaachia wenzangu na kwa vile Wajumbe wangu wa kamati hii wapo watachangia basi nikushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kuuliza maswali machache sana.

Mhe. Spika, mimi swali langu la kwanza nataka niulize kwa nini ashitakiwe nahodha tu wakati ripoti imependekeza na mmiliki naye ashitakiwe? Kwa sababu ukisoma ripoti ya Mhe. Waziri aliyoitoa asubuhi katika *presentation* yeye anapendekeza nahodha ashitakiwe, lakini ripoti hii ya wataalamu inasema nahodha na mmiliki wa meli. Sasa kuna huruma gani Mhe. Waziri aliyoifanya au sababu zipi huyu mmoja akamtoa.

Lakini sababu nyengine ukiangalia hii *presentation* ya Waziri pamoja na hii ripoti ya kitaalamu, meli imezama kwa sababu nne, sababu mbili zinachangiwa na nahodha na tajiri, sababu mbili zinachangiwa na serikali. Sasa Mhe. Waziri haoni kwamba hapa itakuwa ripoti hii ni *bias* kwamba meli imezama kwa sababu nne, sababu mbili zimechangiwa na nahodha na tajiri, mbili zimechangiwa na serikali, lakini anashitakiwa mmoja, huoni kwamba hapa itaonekana wazi wazi kuwa hii ripoti iko *bias.*

Halafu swali jengine Mhe. Waziri katika ripoti yake amesema kwamba meli za *land in craft* kwa mujibu wa sheria ya mkataba wa kimataifa wa *SOLAS* haziruhusiwi kuchukua abiria. Lakini kwa nini serikali ikawa inatoa ruhusa au leseni kwa meli hizi kuchukua abiria wakati inajuwa kwamba ni kinyume na mkataba wa kimataifa wa *SOLAS.*

Mhe. Waziri, katika hatua ambazo ameona kwamba azichukue ili kuondoa matatizo haya, ni kuanzisha uuzaji wa tiketi kwa vitambulisho. Lakini uzoefu mfupi tu unaonesha kwamba tiketi hizi hivi sasa zimekuwa ghali na ulanguzi, ukifika pale unaambiwa hazipo wanapewa vijana wala hawana vitambulisho wanauza pembeni na kuwa kero kubwa sana tangu utaratibu huu uanze.

Je, Mhe. Waziri, haoni kwamba ipo haja ya kuangalia tena utaratibu mzuri wa kuuza tiketi badala ya huu ambao umeleta kero kubwa sana wala haujapunguza tatizo la mrundikano wa abiria katika meli.

Kwa sababu Mhe. Spika, tokea utaratibu huu uanzishwe bado meli zinapakia watu wengi kupita kiasi kuliko hapo zamani, bado meli zinapakia mizigo mingi zaidi kuliko hapo zamani. Kwa hivyo, Mhe. Waziri haoni kwamba utaratibu huu haujatatua tatizo lakini umezidisha tatizo.

Lakini jengine Mhe. Waziri amegusia katika ripoti hii ya wataalamu inasema kwamba, meli inatakiwa itembee kwa muda wa miaka 20, sasa kama meli inatakiwa itembee kwa muda wa miaka 20, kwa nini sisi tunatafuta watu tuwauzie meli zetu ambazo toka kununuliwa zinafika miaka 40? Kwa nini tuwe na azma ya kuuza vitu vibovu wakati tunajua kwamba meli ikifika miaka 20 inatakiwa iwe *written off*. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa kuuliza maswali.

Mhe. Spika, wakati Waziri akiwasilisha taarifa hii kwenye ukurasa wa tatu ameeleza baadhi ya mambo ambayo ni mapungufu, ameeleza mambo manne, yakiwemo ukosefu wa elimu, kukosekana kwa usimamizi na ukosefu wa vifaa na udhibiti na utaalamu mdogo. Lakini ni kwa sababu imetokea shughuli hii au janga hili la meli hii ya *LCT*. Fatih.

Mimi ninahakika kwamba karibu meli nyengine zote mapungufu haya yapo, yaani ukosefu wa vifaa pamoja na mambo mengine. Kwa hivyo, swali langu ni kwamba lisingetokea hili, maana yake ni kuwa tungeendelea hivi inavyoendelea hivi sasa na wala wizara isingetanabahi. Sasa wizara hii majukumu yake makubwa ni yepi kama haya yote yanaonekana hivi sasa kabla ya hapa hayakuwepo, kwa kweli yalikuwepo. Hivyo, wizara inaonekana haiko makini katika hili.

Mhe. Spika, kama hilo halitoshi Mhe. Haji Faki Shaali ametaja hatua ambazo zimetajwa humu zitakazochukuliwa za kisheria na kinidham. Katika *Executive Summary* ya Mhe. Waziri na mimi naita hivyo. Kwa kweli hii ni kubwa, maana watu wengine ukiwapa ripoti na kuona kuna *pages* 50 na nyengine ya *pages* 8 basi atasoma ile ya *pages* 8, ile ya *pages* 50 anaona imeshakuwa *condensed* kwa hapa.

Kwa hiyo, nauliza tena ni sababu zipi hasa ambazo Mhe. Waziri ameona asifuate mapendekezo ya kamati au tume, kwamba tume inasema mmiliki ashtakiwe na katika *Executive Summary* ya Mhe. Waziri hakusema hivyo yeye.

Lakini jengine nilitegemea ripoti hii ya Mhe. Waziri hatosema kwamba hatua za kisheria ziwe hizi na zile. Mimi nilikusudia kwa sababu yeye ndiye mtu wa mawasiliano. Kwa hivyo, yeye kama ni kushtaki atashtaki yeye na atwambie kwamba nafanya hiki na kile na wala sio patafanywa hivi au anapendekeza pafanywe hivi na vile.

Mhe. Spika, haya ni mapendekezo ya kamati au tume ameletewa yeye, sasa yeye atuambie ameyakubali au ameyakataa au yepi ameyakubali na yepi amekataa. Kwa sababu hili bado ni kitandawili, yaani ni mpira ambao hajulikani alicheza rafu ni nani na wala haiwezekani. Ilivyokuwa ni timu ni mbili basi lazima kuna mmoja ambaye aliyecheza rafu, *referee* amepiga kipenga mpira upigwe wapi sasa na hii habari ya mpira udundwe imeshapitwa na wakati. Kwa sababu kudundwa maana yake ni suluhu ambayo haijulikani nani amefanya kosa.

Kwa hivyo, hapa kuna ripoti mbili na mmoja mapendekezo ambayo amepelekewa Mhe. Waziri. Kutokana na hali hiyo Mhe. Waziri, atuambie mapendekezo haya tufuate yake yeye au ya kamati ama tume.

Mwisho katika suala la uimarishaji wa taasisi kwenye ukurasa wa tano. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ndio wizara pekee za kiufundi au miundombinu. Kwa hivyo, wizara hizi ndizo zinazobeba maisha ya watu. Hivi sasa bila ya hizi boti bila ya shaka serikali ingeshindwa usafiri wa Unguja na Pemba pamoja na Dar-es-Salaam. Kwa hiyo, umuhimu wa meli hizi ni mkubwa sana, lakini si umuhimu peke yake na usalama za meli hizi.

Mhe. Spika, unapoiruhusu meli ya mizigo ikajengwa ikawa ya mizigo na abiria, hatuoni kwamba ni makosa ya makusudi ya kusababisha hatari kwa nini serikali iruhusu jambo hili.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kuna hizi taarifa ile ambayo amewasilisha Mhe. Waziri, lakini baada ya kuiangalia tukaona Wajumbe wanaweza kutaka kuona zaidi ndani kuna nini, basi afisi imetayarisha sehemu ya ripoti ambayo kimsingi ndiyo ripoti yenyewe. Kwa sababu lile buku ndani vimo viambatanisho pamoja na mambo mengine, sasa tukatengeneza kitu hiki ambacho kina *pages* 51.

Kwa hivyo, nia hasa ilikuwa tuwatengenezee nondo, kwa sababu hii ni wizara ya mambo ya ufundi, sasa na lazima Wajumbe wawe mafundi. Hivyo, ni vyema tuwatengenezee nondo, ili waweze kuuliza vizuri juu ya taarifa hii aliyotuletea Mhe. Waziri. Kwa kweli hata Mhe. Waziri hakujua kwamba tunatengeneza kitu kama hiki kwa Wajumbe, lakini tumeoa katika lile buku ambalo amelionesha pale, kwa ajili ya kuwatengenezea *equipments* za kufanyiakazi, hiyo ndio namna yenyewe ilivyokuwa. *(Makofi)*

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza maswali machache ambayo wengine wenzangu bado hawajayafikia.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia ripoti ingawa imechelewa sana na wala sijui sababu yake itakuwa nini? Na hilo ni moja ya swali nataka aje atujibu. Lakini tunashukuru kwamba ripoti imefika.

Katika watu ambao wanamasikitiko makubwa kutokana na hili ni mimi kwa hiyo naomba univumilie kidogo.

Pamoja na mengi yaliyomo humu Mhe. Spika, nataka kujua ripoti kwa mujibu ilivyoorodhesha mambo yake yote watu waliokuwemo, walioshiriki pamoja na

mambo mengine, basi hili pia linanipa masikitiko kwamba mimi sikutajwa na wala nisitajwe kama Zakiya, lakini tulikuwa na Kikosi chetu cha *Red Cross*, sasa sijui hawa hawakuhusika au pengine na hao ambao waliokuwa wakifanya uchunguzi hawakujua kulikuwa na hicho kitu. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri atakapokuja atuelekeze.

Swali jengine ni kwamba kwa kadri ya muda mfupi tuliipata hii ripoti kwa bahati mbaya ni kubwa na tuko kwenye kiza, lakini tumejitahidi hivyo hivyo. Bodi hii iliyoundwa ilikuwa ni kubwa sana kwa utafiti wa awali. Sasa Mhe. Waziri haoni kama hii ripoti ni nyepesi mno kulinganisha na tukio lenyewe, kwa sababu kuna baadhi ya wahanga tuliwapata pale kwenye tukio na walisema maneno tofauti na haya yaliomo humu na wala sitaki niyaseme kwa hivi sasa kwa sababu hizi ripoti ndio bado.

Mhe. Spika, pengine kutokana na hizi *rank* za hii bodi yake, haoni kama imesababisha kuwa ripoti iwe nyepesi kulingana na tukio.

Jambo jengine ni kuhusu tofauti ya maelezo ambayo yako kwenye ripoti ya Mhe. Waziri na ile ambayo iko na *pages* 19 inayoelezea idadi ya abiria na kiwango cha mzigo, sasa sijui ipi sahihi. Kwenye ripoti ukurasa wa 19 inasema kuna abiria 25 na mzigo tani 79, lakini kwenye ripoti ya Mhe. Waziri kuna tani 55, sasa sijui ipi sahihi.

Vile vile, ni kuhusiana na hatua zipi watachukuliwa hata hawa wahusika pengine wa Dar-es-Salaam na sehemu nyengine, kwa mujibu nilivyosoma hakukuwa na umakini kwa mtu na kazi yake. Kwa sababu kwenye ripoti humu kuna suala zima la kiwango cha mzigo kinapimwa *manual* wameandika hivyo.

Sasa hivi ni sahihi tu kwamba watizame tu kwa macho na kujua kuwa mzigo huu ni tani 2 au 10. Kwa maana hiyo, haoni Mhe. Waziri hiyo ni *loophole* ya kuingiza vitu vibaya kama vile madawa ya kulevya au silaha na atalichukulia hatua gani hilo.

Mhe. Spika, suala jengine linahusiana na fidia ambayo imetajwa kwamba wamiliki watatakiwa wawalipe hawa vijana. Kwa kweli mimi ninaye mdogo wangu ambaye ni muathirika wa hili nashukuru yupo hai, lakini amepoteza karibu mtaji wake wote wa shughuli zake za kimaisha.

Kwa hivyo, ni utaratibu upi sahihi ambao utakaotumiwa, ili tuwaweze kuwaelekeza vijana pamoja na jamaa zetu katika kufuatilia, kwa sababu kwa kiasi fulani huko nyuma wenyewe tayari wameshakwenda mbio na kupiga mpira sana na wameamua kumuachia Mwenyezi Mungu. Lakini kwa kuwa leo

limekuja hapa, basi tunataka kujua ni utaratibu upi na kwa namna gani wataweza kupatiwa haki yao.

Mhe. Spika, mwisho naomba kutoa ombi kwa wananchi naomba uniruhusu kwa sababu hili si swali, isipokuwa ni ombi kwa wananchi. Kwa sababu ripoti ya Mhe. Waziri kuhusiana na suala la fidia. Kipengele hicho kinazungumzia sheria kwamba inawatambua wale tu walioingia melini, ambao wakiwa na tiketi zao halali kama abiria halali na ndio watakaolipwa fidia.

Sasa hapa ninalo ombi kwa waheshimiwa wananchi wetu wa Zanzibar. Mhe. Spika, wananchi wetu wamezoea dezo, kwa sababu vyombo kama hivi huwa wanatoa shilingi 1,000/- au 2,000/- anaingia yeye pamoja na watoto wawili au watatu, yaani anakuwa hayumo kwenye hesabu na wala hana tiketi halali. Kwa hivyo, nawaomba sana hii dezo inatumalizia uhai wa watu na roho zao.

Kutokana na hali hiyo, nawaomba hili waliache kwa sababu hata kama inapotokea hatari kama hii ikiwa kuna watu wamekufa au wameathirika kwa namna moja au nyengine, basi hawatopata haki zao.

Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza baadhi ya maswali katika tukio hili la kusikitisha. Mimi nakwenda moja kwa moja kutokana na utaratibu wa kikazi katika bandari iwapo meli itazama hali ya kuwa imeshafunga gati. Je, nani muhusika mkuu, nani atakayehusishwa zaidi.

Swali langu la pili ni kuhusiana na ripoti yenyewe ilitaja kwamba kulikuwa na kitabu kinachoitwa *Stability Data Book* lakini kimeandikwa kwa Lugha ya Kifaransa. Mimi nauliza kuwa kuandikwa Kifaransa ndio vioja, yaani hakijulikani au vipi? Je, wizara haiwezi kupata mtaalamu wa Lugha ya Kifaransa na kukisoma hiki kitabu? *(Makofi)*

Mhe. Spika, swali langu la tatu ni kuhusiana na kujua abiria wanaoingia katika boti hizi kwa kuweka utaratibu wa kutoa kitamulisho. Kwa hivyo, nauliza hili lilitangazwa au lilifanyiwa utafiti, kwa sababu watu wengi wanaokwenda pale kwa kweli wanaazima wengine, kama mtu hana basi anaazima na kuandikiwa tiketi kwa jina unalosema.

Vile vile, tiketi nyengine zinauzwa na kuandikwa tu. Kwa mfano Rashid Juma Ali na halafu unauziwa, yaani jina moja tu, sasa hawa watajulikana vipi? Kwa hivyo, nauliza utaratibu huu ulifanyiwa utafiti au ulitangazwa kwamba

utasaidia? Pamoja na hilo pale wanapoingia abira ambao hawana tiketi, nani muhusika au dhamana ni mmiliki wa boti au Shirika la Bandari.

Mhe. Spika, kwenye ripoti napenda kuuliza swali jengine tokea kumaliza hii ripoti na wala sio kuletwa hapa, kwa sababu hapa mpaka wewe mwenye Mhe. Spika, umekiri kuwa umechelewa sana. Lakini tokea siku iliyomaliza wakaisoma hao wahusika ni kifaa gani ambacho kilichoongezwa, kwa ajili ya kuokoa maisha, utaratibu gani uliobadilishwa wa kuondoa hizi dosari na nani aliyewajibishwa kwa kukosea katika utaratibu mzima wa usalama wa chombo baharini.

Mwisho Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa Kitengo cha Kutoa Haki ni Mahakama. Je, serikali ina kigugumizi gani kulipeleka suala hili Mahakamani? Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Abubakar Khamis Bakary:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza maswali kidogo tu. Kwanza naishukuru afisi yako Mhe. Spika kwa kutuletea *summary* ya huu uchunguzi uliofanywa.

Lakini nafikiri utaratibu ulivyo ni kwamba Waziri anayehusika anapokuja na *summary* yake, basi ni lazima na ile ripoti atufunganishie ili tuweze kuyafahamu zaidi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hilo ulilifanya ingawa haikuwa yote, lakini tunakushukuru kwa msaada wako huo.

Mhe. Spika, badala ya hiyo, nauliza swali la mwanzo *summary* hii tuliyoletewa na ripoti ya Mhe. Waziri zinatofautiana na wala hazikubali kabisa. Sasa ipi ya kuiyamini ile bodi iliyochunguza au Waziri alotuletea *summary*? Kwa maana hiyo, yepi tuchukue kwamba ndio mapendekezo halisi ya tukio lote lilotokea?

Swali la pili, hii meli kwa mujibu wa utaratibu ni kwamba iliundwa mwaka 1965, lakini mwaka 1979 ilifanyiwa marekebisho, ili iwe ya mizigo tu. Lakini mmiliki baada ya kuinunua yeye alibadilisha tena na kuwa ya mizigo na abiria bila ya kupitia utaratibu wowote ule. Kwa hivyo, mmiliki kwa kiwango kikubwa kabisa naye ni mkosa. Sasa kwa nini mmiliki hakuwekwa kwenye orodha ya hao washtakiwa?

Tatu, ni kuhusu bima hata ukenda ku-*insure* gari yako, ambayo karibu itakuwa *write off*, basi Shirika la Bima mara nyingi huwa hawataki tena. Sasa ilikuwa meli hii Shirika la Bima wakakubali kumfanyia bima *almost* mara tatu ya kiwango cha bei. Je, hakuna tatizo lolote baina ya bima na hawa watu wanaohusika na kuna hatua gani ambazo Shirika la Bima limechukuliwa?

Mhe. Spika, swali la nne, ni kwamba ukisoma hii ripoti ambayo Baraza wametuletea utaona serikali mmiliki na nahodha wote ni wakosa. Serikali kuna Mkaguzi na Mrajis ambao wameelezwa katika ukurasa wa 26-27, Mkaguzi hakukagua mwahala ambamo anatakiwa akaguwe na Mrajis hakutekeleza wajibu wake. Lakini na mmiliki nae hakufanya alichotakiwa afanye. Kwa hivyo, wote hawa wamesababisha watu na mali zao kuathirika. Ni sababu ipi inayofanya kusema kwamba Waziri pendekezo lake kwamba ashitakiwa nahodha peke yake? Asishitakiwe mmiliki na wasishitakiwe Mrajis na Mkaguzi ambao nao walichangia sehemu kubwa kupoteza mali za hawa watu na abiria wengine kufa.

Mhe. Spika, swali la mwisho Mhe. Waziri anaweza kutwambia hizi meli zetu zinazokwenda baina ya Unguja, Pemba na Dar es Salaam, kila meli akatutajia ni watu wangapi wanaoruhusiwa kisheria? Kwa sababu kama Serengeti inaweza ikachukua watu 1,500 mbali mafenesi, kuku, mikungu ya ndizi na kadhalika. Kwa hivyo, idadi hii ndio kweli idadi ya abiria au basi tu Mkaguzi na Mrajis na watu wengine wanaachia kiholela meli kama hizi?

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi hii na mimi nikapata nafasi ya kuuliza maswali mawili matatu juu ya taarifa hii ya serikali juu ya kuzama kwa meli ya MV. Fatih.

Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza serikali kuwasilisha taarifa hii hapa Barazani juu ya kadhia hii ambayo kwa kweli wengi imetusononesha pamoja na kwamba taarifa hii imechelewa kufika hapa, lakini taarifa ndio tumeiona na kwa kiasi fulani iko wazi na inaonekana ni jinsi gani bodi hii iliyoundwa imefanya kazi zake vizuri.

Mhe. Spika, uchunguzi uliofanywa unaonesha dhahiri kwamba kulikuwa na uzembe katika suala zima la kusimamia shughuli nzima hizi za usafiri ama wa chombo chenyewe au usimamizi wa taasisi zinazohusika na usalama juu ya vyombo hivi pamoja na abiria. Taarifa inaonesha kwamba kuna baadhi yao wanahitaji kushtakiwa, lakini wengine kuchukuliwa hatua za nidhamu na wengine kulipwa fidia.

Mhe. Spika, mimi nataka kumuuliza Mhe. Waziri, je, katika suala zima la malipo ya fidia kwa waathirika anaelewa kwamba waliopoteza mali zao hadi leo hii hawajalipwa fidia zao.

Pili, ni kwamba katika sheria hii Nam. 5 ya 2006 inatoa muda gani wa kulipwa fidia inapotokezea suala kama hili.

Tatu, unapozungumzia kulipwa fidia Mhe. Waziri unakusudia kulipwa vipi juu ya watu hao.

Nne, kama mmiliki wa meli ameshindwa kulipa fidia kwa wakati ni hatua zipi ambazo anapaswa kuchukuliwa.

Tano, katika utekelezaji wa shughuli hizi ambapo bodi inawezekana kuwa imetumia gharama, je, ni kiasi gani cha fedha kilichotumika hadi kukamilika kwa uchunguzi huu? Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Spika, ahsante na mimi naomba nimpongeze Mhe. Waziri na pia bodi ambayo imechunguza hii kadhia na kweli inaonekana imeandaa ripoti nzuri sana.

Mhe. Spika, suala langu la kwanza ni kwa nini Mkaguzi wa meli aliyeikagua meli kwa uzembe na kuipotosha Afisi ya Mrajis asifutiwe leseni na baadae kushtakiwa.

Mhe. Spika, ni chombo gani katika serikali kinamteua huyu Mrajis wa Meli?

Pia, tuliambiwa kwamba Afisi ya Mrajis wa Meli haina utaalamu na uzoefu wa kutosha katika ripoti hii na kwa sababu jambo hili sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mara nyingi tumemshauri Waziri juu ya umuhimu wa kuongeza utaalamu wa kitengo hiki, lakini bado ameonekana hajazingatia ushauri huu hadi ilipotokea ajali. Je, ni lini na kwa vipi anategemea kuwaongezea mafunzo wafanyakazi wa Afisi ya Mrajis?

Je, afisi hii haina afisi inayotambulika na vifaa vizuri au nyenzo za kufanyia kazi?

Kwa kuwa tumeambiwa katika ripoti hii kwamba ajali imetokea bandarini Malindi na ikachukua masaa 5 kabla ya shughuli za uokozi hazijaanza na pia tumeambiwa Shirika la Bandari halikuwa na mpango wa dharura wa uokozi pia hata taa kulikuwa hakuna. Je, hali ikoje hivi sasa kuna mambo yamerekebishwa?

Pia, tumeambiwa katika ripoti hii kwamba hali ya usafiri wa baharini hivi sasa meli zinazokwenda Pemba sio nzuri, ni kweli meli zinaonekana kuchakaa, zina joto jingi, abiria hupakiwa bila ya kiwango. Je, pamoja na ajali iliyotokea, lakini bado suala hili linaendelea tunasubiri ajali nyengine itokee ndio tuunde tume na kuleta ripoti hapa Barazani?

Mhe. Spika, swali langu la mwisho, kwa mujibu wa ripoti hii nasema aidha mmiliki wa meli baada ya kuchukua meli na kuja nayo Zanzibar alipeleka Mtoni kwa kuifanyia matengenezo madogo madogo na mabadiliko yasiyo rasmi kutoka meli ya mizigo na kuwa meli ya abiria, mabadiliko hayo yalifanywa chini ya usimamizi na maelekezo yake mwenyewe na bila ya kufuata utaratibu wa kisheria uliowekwa.

Je, mambo haya yanayofanyika Mamlaka ya Usimamizi wa Serikali ilikuwa wapi?

**Mhe. Abass Juma Muhunzi:** Mhe. Spika, nakushukuru sana, swali langu la mwanzo linahusu muhutasari huu uliotolewa na Waziri, kifungu cha 10 (b) ambacho kinasema, "ilipotokea ajali nahodha haikuipeleka meli kwenye mchanga", lakini vile vile, ziko taarifa nyengine tunazozipata ni kwamba nahodha aliomba ruhusa ili aipeleke kwenye mchanga na hakuruhusiwa. Kwa sababu hili lime-*appear* kwenye taarifa na kwa sababu upande wa pili wa taarifa tunapata taarifa hizo, kwa sababu haya ni mambo yametuhusu sote na kila mmoja alikuwa anatumia njia zake kufanya uchunguzi.

Je, Baraza hili kabla ya kupitia Kamati yake ya Mawasiliano na Ujenzi haioni haja ya kulichunguza suala hili la kutoipeleka meli kwenye mchanga ikatuletea ripoti hapa? Kwa sababu kitendo cha kuipeleka meli kwenye mchanga inaonesha kwamba ingeweza kuzuia maafa haya makubwa. Hilo la kwanza.

Mhe. Spika, tulipata taarifa kwamba meli ilizama kwa muda mdogo sana, ilipopindukia tu ilizama ambapo inakuwa si kawaida ya meli hasa zinazochukua abiria. Je, swali langu Mhe. Spika, ni matatizo gani ya kiufundi yaliyotokea au ni aina gani ya meli inayoweza kuzama kwa dakika chache kama hizo wakati inaruhusiwa kuchukua abiria?

Swali langu la tatu, kwenye muhtasari wa kifungu cha 7, meli haikuwa na usalama wa kiufundi tokea iliponunuliwa. Sasa swali langu ni kwamba ikiwa leo watu wananunua gari tu, wanaambiwa wanunue gari ya mwaka fulani, gari sijui ipite kwenye *JAA inspection* na mambo kama hayo. Je, ni kwa nini inaruhusiwa kuingiza meli hapa ambayo inachukua abiria wengi pamoja na mali za watu wengi bila ya kuwa na utaratibu wa kuweka viwango ambavyo meli hiyo inatakiwa kununuliwa? Na kwa nini baada ya kununuliwa iruhusiwe kuingia na kufanya kazi?

Swali langu jengine ni suala la usajili ambalo wenzangu wameshazungumza. Lakini suala linalotokana na muhutasari huu huu kifungu cha 10(e) la chelezo kwamba, haikupelekwa chelezoni. Hapa tunaambiwa kwamba kuna matatizo ya marekebisho ya sheria na kanuni, hakuna sheria ambayo inamtaka mwenye

meli kuipeleka chelezoni kwa wakati muwafaka na kama hakuipeleka kwa nini iliruhusiwa meli hii kufanya kazi? Kosa ni la nani katika hapa, ni aliyekuwa hakupeleka au aliyeruhusu meli iliyokuwa haikupelekwa kuchukua abiria.

Swali jengine ni suala linalohusu uokozi nalo limo katika muhutasari Nam.11. Mhe. Spika, kuna utaratibu wa wanaofanya kazi katika meli hupewa *training* ya uokozi na hawa watu wa Idara ya Uokozi (*FIRE*) na inafanya hivyo kwa meli za serikali. Je, matakwa haya ya kufanya mazoezi kwa uokozi mbali ya ile kuwa na vyeti vya uokozi yale mazoezi tu, kwa uokozi ni jukumu la mwenye meli au ni jukumu la serikali kuwaambia wenye meli kuwa lazima wafanye hivyo. Je, ilifanywa hivyo au haikufanywa? Kama haikufanywa nani ambaye ana kosa katika hili?

Suala jengine limo katika muhutasari wa 13 kwa sababu imeelezwa hapa kwamba yote haya yanayofanywa yanafanywa kwa ajili ya kuimarisha shughuli za meli ili yaliyotokea yasije yakatokea tena. Sasa swali, kwa sababu tunaziona meli nyengine nyingi zinazokwenda zinakwenda kwa matatizo, kama tumepata hiyo taarifa ya Meli ya *Seagull*, tunaiona meli ya Serengeti ambayo kwa kweli iko katika hali ambayo kila mmoja sasa hivi tunashituka sana. je, ni nini kimefanywa baada ya tukio hilo kwa hizo meli nyengine? Haya mapungufu yanayoonekana mpaka yakasababisha ajali hii je, hayatokea tena katika meli hizi nyengine, mapungufu hayo hayako? Na tutajitosheleza vipi sisi Wajumbe tuone kwamba mapungufu haya hayamo katika meli hizo nyengine.

Je, Mhe. Spika, huoni kwamba bado kamati yako ya Mawasiliano na Ujenzi kuna haja ya kufanya kazi kuona kwamba haya yaliyokwishatokea hayatokei tena ikatuletea ripoti hapa?

La mwisho kabisa Mhe. Spika, ni suala la mahusiano baina ya *operators* na Idara ya Bandari au Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Yapo manung'uniko ya kwamba kuna aina fulani ya migongano kati ya wenye meli pamoja na watendaji wa Wizara ya Mawasiliano ambao wanashughulika na meli. Maoni haya yanakuja aina mbili, wanasema kwamba ziko meli huwa zinapendelewa na ziko meli huwa zinafanyiwa matatizo zinapokuwa zinataka kufunga gati au zinapotaka msaada kwa ajili ya maafa ambayo yanatokezea.

Kwa sababu hili ni suala ambalo nalo linatakiwa kutolewa kauli hapa Mhe. Spika, huoni kwamba iko haja ya kuwakutanisha hawa kupitia hiyo hiyo kamati yetu ya Baraza? Kwa sababu hili ni suala la *over sites* na Kamati ya Baraza ndio ambayo inashughulikia hivyo. Kwa hivyo, ikawakutanishe *operators* pamoja na watendaji husika wa Wizara ya Mawasiliano ili kuona kwamba ikiwa kuna tafauti zinasafishwa ili kusije kukatokezea tena matatizo yoyote katika harakati hizo za meli. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Moh'd Ali Salim:** Mhe. Spika, ahsante sana mimi naomba nianze kuuliza swali la kwanza. Mhe. Spika, kwa kuwa maafa hayatokei baharini tu, lakini maafa pia yanaweza yakatokezea angani. Hivyo, kuna hatua gani zilizochukuliwa za kuhakikisha kuwa maafa ya angani hayatokei kama yalivyotokea haya ya baharini?

Mhe. Spika, swali jengine ambalo kuna walioliuliza, lakini mimi nataka niliulize kwa njia nyengine hili suala la meli zinazochukua watu kupeleka Pemba na kurudisha Unguja. Je, Mhe. Waziri, baada ya tukio hili lililotokea ni hatua gani atakazozichukua za makusudi za kukagua upya meli zote zilizopo hapa Zanzibar?

Jengine ni kwamba kwa kuwa ripoti inasema nahodha alishauriwa na abiria aipeleke kwenye mchanga meli na akakataa. Je, ni sababu ipi kwa mujibu wa uchunguzi iliyosababisha uamuzi huo?

a) Ukaidi?
b) Kughumiwa?
c) Alikatazwa na mamlaka?
d) Je, aliwahi kupimwa akili baada ya tukio?

Mhe. Spika, suala jengine ni kwamba serikali itachukua hatua gani za kufanya marekebisho katika uokozi katika bandari ya Malindi na katika bandari ya Mkoani?

a) Hatua za dharura
b) Hatua za kudumu

Mhe. Spika, suala linalofuata meli ikimaliza muda wake au ikiwa haifai tena kutumika hapa Zanzibar, jaa lake liko wapi la kutupwa?

Mhe. Spika, suala langu la mwisho ni kwamba bodi imeona kuwa meli imesajiliwa kinyume na sheria Nam.5 ya 2006, kwa sababu wakati wa kutaka usajili wa kudumu nyaraka muhimu hazikupatikana. Haionekani kama kusajiliwa huku kinyume na utaratibu ndio kulikosababisha ajali hii itokee. Kwa hivyo, hawa wanaohusika na mambo haya ndio waliokuwa wachukuliwe hatua hizo.

**Mhe. Aziza Nabahan Suleiman:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii niulize maswali mawili matatu haidhuru maswali mengi yameshaulizwa, lakini bado na mimi naweza nikapata nafasi nikauliza kidogo.

Mhe. Spika, katika ripoti tumeambiwa kwamba meli ilikaguliwa na mkaguzi na Mrajis akakubali kuisajili, lakini hapa tunaambiwa kwamba hakuna nyaraka

yoyote ya meli ile kwa Mmiliki imezama na meli kwa Mrajis hakuna, kwa Mkaguzi hakuna, sasa hii kazi ilifanywa vipi au kuna nini hapa Mhe. Waziri naomba anisaidie.

Mhe. Spika, suala jengine ni kwamba meli imeundwa 1965, lakini hapa tumeambiwa meli imeundwa 1979, huu ni uongo dhahiri tulioelezwa na mmiliki wa meli. Je, tutamchukulia hatua gani kwa kusema hivi?

Mhe. Spika, jengine ni kwamba kuna kawaida kuwa meli za serikali zilikuwa kila mwaka zinakwenda kuangaliwa. Je, meli hizi tulizokuwa nazo zinafanyiwa kazi hiyo ya kutizamwa kila mwaka kama meli hizi zinaweza kuendelea na kazi? Mhe. Spika, lakini ajali ikitokezea barabarani dereva hukamatwa je, wahusika wa tukio hili walichukuliwa hatua gani baada ya kwishakutokezea hili tatizo au zile roho za watu na mali zao zilikuwa zimepotea bure?

Mhe. Spika, meli mbovu ziko nyingi sana na tumeshapiga kelele sana, je, Mhe. Waziri, atazifutia leseni zile meli zote zitakazohakikishwa kama ni mbovu na hazitafanya kazi tena kwenye bandari yetu?

**Mhe. Juma Duni Haji:** Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana mimi nina suala moja tu, lakini nadhani linakwenda kwa wizara yenyewe. Ukisoma ripoti ya Mhe. Waziri ukurasa wa 3 ameweka mapendekezo ya hatua zinazochukuliwa kwa ruhusa yako naomba ninukuu.

> "Hatua za kisheria za kuchukuliwa kwa wahusika, hatua za kinidhamu za kuchukuliwa kwa wahusika, malipo ya fidia kwa waathirika, marekebisho ya sheria na kanuni, uimarishaji wa taasisi na utekelezaji wa usimamizi"

Mhe. Spika, mimi nimeshawahi kuwa Afisa wa Serikali na ninajua katika kupewa dhamana huwa tunaapa mimi fulani bin fulani nitafanya kadhaa, sasa kuna kitu tunaita *responsibility* na *accountability*. Hivyo, namuuliza Mhe. Waziri, kwamba wengine wote wanachukuliwa sheria hakuna katika wizara hata mmoja anayewajibika? Kwa sababu kwa vyovyote vile wizara inawajibika kwa suala hili au utaratibu huu hivi sasa serikalini haupo?

**Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja:** Nashukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi nataka kuuliza swali ambalo halijaulizwa, naona mengi yameshaulizwa.

Mhe. Spika, ninachotaka kuuliza ni kwamba wakati hii meli ilipozama imeokolewa ni kiasi gani cha gharama zilizotumika katika kuiokoa?

Mhe. Spika, ni nani anastahiki kulipa gharama hizo na kwa sasa gharama hizo zimelipwa na nani?

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, kwa kweli mimi sitokuwa na maulizo isipokuwa nitakuwa na ushauri.

Mhe. Spika, pamoja na yote yaliyozungumzwa, hayo mimi nichukue nafasi hii kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwasilisha ripoti hii juu ya kwamba imechelewa, lakini natumai ni ripoti nzuri na imekamilika.

La pili, nichukue nafasi hii Mhe. Spika, kuwashukuru wale wote kwa njia moja au nyengine waliosaidia katika masuala ya uokozi na misaada mbali mbali mara tu baada ya kutokezea ajali hii.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ameeleza humu mna mapungufu, mna mapendekezo, mna ushauri, mna marekebisho ya kanuni na kadhalika. Mhe. Spika, kutokana na umuhimu wake masuala haya ningemshauri Mhe. Waziri kama yapo ni sawa, lakini kama hapana basi ningemshauri Mhe. Waziri kwa makusudi ili utekelezaji uwe wa haraka na mzuri na uweze kuonekana. Mimi namshauri Mhe. Waziri kwamba awe na kitengo katika wizara yake ambacho kitashughulikia masuala haya kwa sababu masuala ni mengi na yanataka kushughulikiwa na kila mmoja lina umuhimu.

Mhe. Spika, katika kuyashughulikia haya, pendekezo langu baada ya kuundwa chombo hicho basi yale mapungufu au mapendekezo na kadhalika yaweze kuorodheshwa na kupangwa kwa kipaumbele, kwamba haya yachukuliwe hatua mara moja, haya yafuatie na haya yafuatie. Nafikiri Mhe. Waziri ameshanifahamu, ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi:** Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii, mimi masuala yangu yatakuwemo katika maelezo na yatatoka masuala lakini nitauliza, je, baada ya yote hayo yaliyotokezea Mhe. Waziri haoni kama ni busara kuweka *traffic* ya polisi katika bahari kwa sababu katika bahari kuna kitengo cha polisi, lakini *traffic* kama nchi kavu kwani wanaweza kuifuata meli, wanaweza kuisajili meli, wanaweza kutoa masuala katika meli na kuuliza kila kitu. Mhe. Spika, ni vizuri kitengo cha polisi akashirikiana na *IGP* kikafufuliwa halafu wakapewa boti yao wakawa wanafuatana na wanaweza kuleta habari nzuri.

Mhe. Spika, ni kwamba hatuna kikosi cha uokozi, si kila anayeweza kupiga mbizi ni muokozi, wako watu wanapiga mbizi kwenye maziwa hawawezi kuokoa meli, wako watu wanapiga mbizi katika mito hawawezi kuokoa meli,

lakini kupiga mbizi kitu kimoja na kuokoa kitu chengine. Kwa hivyo, Mhe. Spika, sio kila mpiga mbizi ni muokozi, huwa kunakuweko watu kitengo kinafundisha watu maalumu wanaitwa *frogmen* basi anaweza kwenda katika bahari meli imezama basi akafungua meli, vyumba akajua nini anafanya, lakini sio msalie Mtume huyu ameshakufa mtoe, hiyo sio wanakuwa wameshapewa mafunzo. Mhe. Spika, nchi zote zenye bahari na bandari wanaweka kikosi kinaitwa *frogmen*, KMKM si waokozi wanaweza kuokoa, lakini si waokozi kama *frogmen* na si kila *diver* mzuri anaweza kuokoa.

Mhe. Spika, kama nilivyokwambia ma-*diver* wengi wana-*dive* katika mito na maziwa lakini hawawezi kuokoa vitu. (*kicheko*)

Sasa kama ilivyokuwa gari zinapasishwa na meli zipasishwe, kama ilivyokuwa gari zinafuatwa na *traffic* na meli zifuatwe na *traffic*, kabla watu kwa mfano watu wa Somalia hawajaanza kuja hapa kuanza kuizuia meli ya Pemba iliyokuja Unguja bure wakachukua embe. Hamna kitu mle, ahsante Mhe. Spika, nakushukuru.

**Mhe. Spika:** Maziwa ni kama vile *Lake Victoria* na *Lake Tanganyika*. *(Kicheko)*

Nafikiri tukubaliane kwamba masuala haya ni mengi sana na ni vyema Mhe. Waziri, akapata muda au kama yuko tayari ataeleza mwenyewe, lakini kwa kweli ni mengi.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kukubali kuwasilisha ripoti yetu hii leo.Pia, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuuliza maswali mazuri yenye msingi wa kuimarisha huduma zetu za meli katika nchi yetu ya Zanzibar ambayo ni ya visiwa.

Pia, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Omar Ali Shehe (Waziri Kivuli, Wizara ya Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi), kwa maelezo yake mazuri ambayo yana muongozo wa kufanyia kazi.

Mhe. Spika, kwa ujumla Waheshimiwa Wajumbe 17 wameuliza maswali, lakini wengi wao wameuliza swali la kwamba kwa nini ripoti imechelewa sana. Naomba nalo hili nilijibu kwa ujumla.

Mhe. Spika, kama inavyojulikana kuwa ajali hii ilitokea tarehe 29/5/2009 na bodi niliiunda na kuizindua tarehe 11/6/2009. Ilifanya kazi kwa mwezi mmoja na nusu. Kwa hivyo, katika Baraza la Bajeti bodi hii ilikuwa ikifanya kazi. Baada ya kuwasilisha ripoti na kitabu umekiona Mhe. Spika, ni kikubwa tabaan

tusingeliweza kuileta katika kikao cha Oktoba. Na kwa sababu niliahidi kwamba ripoti hii lazima niilete Barazani, sikuona umuhimu wa kuitoa pengine katika vyombo vya habari bila ya kuileta Barazani. Sasa baada ya kikao cha Oktoba kwa mujibu wa kalenda za vikao ni kikao cha Januari hii tuliyonayo. Bila shaka tusingekuwa na nafasi nyengine ya kuleta Barazani kabla ya kikao hiki.

Kwa hivyo, Waheshimiwa naomba muelewe nyote kwamba tulichelewa au tulifuata utaratibu wa Baraza na tusingeliweza kuwahi kabla ya kikao hiki cha Januari. Na hatukutaka hii ripoti itolewe katika taasisi nyengine bila ya Baraza hili kupata baraka zake.

Halafu Mhe. Omar Ali Shehe, Waziri Kivuli alizungumzia kuzimika kwa *Seagul* akasema ni tarehe 24, ukweli ni tarehe 25 na tatizo lake ilikuwa ni jenereta wala haikuwa katika shughuli nyengine, bahati mbaya ilikuwa hapo Chumbe na baadae ilifungwa kidogo baadae jenereta zikakubali nafikiri zilikuwa zimepata *heat* kubwa na baadae ikaendelea na safari. Lakini sisi kama serikali tulikuwa tunafuatilia kwa karibu na nilishawaarifu bandari kwamba likiendelea hili tatizo waende wakaivute wailete bandarini, lakini baadae chombo chenyewe kiliweza kufika bandarini salama.

Kuhusu wananchi kutumia vyombo salama na sisi tunaomba hivyo hivyo, kwamba ni vyema wananchi kutumia vyombo salama. Kwa sababu pamoja na unafuu na ugumu wa maisha, lakini bado maisha ni mazuri zaidi kuliko gharama za maisha yenyewe. Kwa hivyo, nawaomba wananchi kupitia Baraza hili wajitahidi sana kutumia vyombo ambavyo vinaaminika na sisi kama wizara tunajitahidi sana kuangalia chombo ambacho ni kizima.

Kuhusu kutekelezwa kwa maoni ya bodi, Ninawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba wizara yetu itahakikisha kwamba mapendekezo tunayafanyia kazi.

Mhe. Zahra Ali Hamad, anasema mabaharia wengi wana vyeti *fake.* Kuna kipindi ilikuwa hivyo, lakini sasa zamani sisi tulikuwa hatutoi vyeti, vyeti vilikuwa vinatolewa na SUMATRA, lakini sasa na sisi hapa tunatoa Mrajis wa meli. Kwa hivyo, tuna hakikisha kwamba mtu ambaye anapata cheti ana sifa za kuwa baharia kwa sababu kuna *grade* nyingi sana za ubaharia. Kwa hivyo, kila mmoja anapata cheti kutokana na daraja yake ambayo amefikia. Tukimjua mmoja mmoja tutawafutia leseni zao kwa sababu hili ni taratibu na zoezi la kudumu.

Kuhusu mmiliki. Hili limeulizwa sana, kwamba kwa nini aliifanyisha kazi bila ya taratibu zinazohusika. Kwanza kuna ripoti ya bodi na kuna ripoti ya waziri,

bodi imeniletea mimi na mimi nikaangalia uhalisia wa mambo yalivyo. Katika suala hili na ndio maana ukaona huko mbele mmiliki hatukumpeleka Mahkamani, tukasema alipe fidia kwa hao waathirika. Kwa sababu habari za kwamba mmiliki kahusika hata ripoti yenyewe inachukuwa kwamba zimetolewa na baharia ambaye kafukuzwa kazi na mmiliki na hapo mwanzo hakusema. Kwa hivyo, inaonekana kama kuna maslahi binafsi au mgogoro wa kimaslahi kati ya mmiliki na baharia wake aliyekuwa wa zamani. Kwa hivyo, sisi tukasema hili kidogo lina mashama katika suala hili.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu alisema ripoti imechelewa, lakini kama nilivyosema mwanzo sababu za kuchelewa ripoti ni hiyo. Lakini pia, alisema nani atachukua hatua za kinidhamu. Kwa wale ambao wako chini ya wizara yetu, watumishi wetu tutawachukulia sisi na kwa nahodha nidhamu tutachukua sisi, lakini kisheria kwa mujibu wa sheria ilivyo ya usafiri baharini, inatakiwa baada ya utoaji wa ripoti hii ndipo hupelekwa Mahkamani, sasa tupeleke mashtaka kwa Afisi ya Mwendesha Mashtaka ili achukuliwe hatua na ndivyo ambavyo tutafanya baada ya ripoti hii kuitoa.

Kuhusu nahodha kusimamishwa kwa muda muwafaka, hatukupenda kuweka muda wa nahodha kusimamishwa leseni yake kwa sababu tunahisi huyu tunampeleka Mahkamani, sasa tukitowa muda wa kwamba miaka miwili au mitatu na Mahakama kule ikasema vyengine itakuwa tumeingia uhuru wa Mahakama. Kwa hivyo, kwa huyu tumeliacha wazi mpaka kesi yake itapokwisha. Lakini kwa hawa wengine mabaharia waliodanganya tumesema mwaka mmoja wazi wazi kwa sababu wao hawendi Mahakamani isipokuwa walishindwa kuisaidia bodi kutoa maelezo ya kweli zidi ya nahodha wao.

Alisema pia, je, kosa hili ni la kukusudia au kwa bahati mbaya? Nafikiri wenye kujua hivyo ni Mahakama, kama ilivyo ajali ya barabarani kwamba ukimpeleka mtu Mahakamani, Mahakama itasema kauwa kwa kukusudia au kauwa bila ya kukusudia. Sisi kama wizara nafikiri hatuna mamlaka ya kusema kosa hili la kukusudia au si la kukusudia.

Halafu aliuliza muda wa meli kufanya kazi. Waheshimiwa Wajumbe hakuna sheria mpaka sasa hivi inayosema kwamba meli ya miaka 50 haifai kufanya kazi. Kwa hivyo, bado hakujawa na sheria hiyo na si Zanzibar tu nadhani karibu mataifa yote. Lakini sasa sisi tutaangalia, je, hii sheria inawezekana kuweka kifungu hiki au vipi, ilimradi meli inatakiwa ifanyiwe *service* na kuna meli za kimataifa za zamani sana zina miaka 60-70 zinafanya kazi, lakini zinatakiwa zifanyiwe *service* bado hakuna muda ambao umewekwa maalumu.

Mhe. Haji Faki Shaali, anasema kwa nini ashitakiwe nahodha tu na sio wengine? Mmiliki ndo keshasema hilo, kwa sababu hiyo ripoti ya tume

imeniletea mimi, lakini bado kuna kadhia ya mgogoro wa kikazi wa maslahi ambao hata afisini kwangu upo kati ya mmiliki na baharia wake aliyekwenda kuchukua meli ambaye alimfukuza kazi baada ya wenyewe kukosana. Kwa hivyo, kidogo tunahisi tusiende tukamuumiza mtu kwa sababu nyengine.

Lakini pia, umesema sababu za kuzama meli ni nne, mbili zetu na mbili za mwenye meli na nahodha. Mimi ripoti imekuja naikubali na ndio maana sikutaka kuficha hata kitu kimoja, nimeleta kitabu kizima kwa Spika, kwamba kila mtu si leo tu asome hata miaka mingine kwamba kilitokezea kitu gani. Kama kasoro zetu sisi tumesema tutachukua hatua kwa wanaohusika, lakini pia hii ripoti tumeichukulia kujiweka sana kwa ajili ya mambo ya baadae ili mambo haya yasitokezee. Nchi yetu tunaijua sote kwamba ni nchi ya visiwa, huwezi kusema hata siku moja kwamba Zanzibar haitatokezea ajali ya baharini hilo haliwezekani, lakini tufanye kwamba ikitokezea basi iwe imetokezea kwa bahati mbaya na hakukuwa na makosa ya mtu au uzembe wa mtu.

Halafu mkataba wa *solar* kwamba unakataza *land craft* kuchukua abiria. Mhe. Spika, mkataba wa *solar* hauzuwii kabisa mbele ya *land craft* kuchukua abiria, inaruhusiwa. Katika ripoti umeona hivyo kweli, lakini ilivyo hapo bodi wamepitikiwa, lakini inaruhusiwa kuchukua abiria bila ya tatizo lolote. Na mabadiliko pia ya muundo wa meli yanaruhusiwa, lakini baada ya ukaguzi maalumu. Kwa hivyo, hili nataka niliweke sana tu kwamba *solar* inaruhusu kuchukua *land craft* yaani kuchanganya mizigo na abiria.

Kuhusu kuuzwa *ticket* kwa vitambulisho Waheshimiwa Wajumbe hili zoezi linatuhusu sote, sisi wizara tunajitahidi tusifeli, lakini na nyinyi Waheshimiwa Wajumbe mna haki na wajibu wa kuwaelimisha wananchi wetu. Mimi nakaribisha mapendekezo yenu kama mnaona hili haliwezekani au gumu tufanye nini ili kupunguza tatizo, basi kama alivyosema Mhe. Abass Juma Muhunzi na nyinyi labda muiambie Kamati ya Mawasiliano watwambie ziuzwe vipi. Kwa sababu tunalolikataa sisi katika meli hii iliyozama ambayo tuliambiwa ina watu 25 haikuwa 25, lakini hata katika ile 25 watu wote hao jina lililoonekana limetoka huku na huku likawa sawa ni moja tu. Majina 24 yote ya Machano, lakini Machano wenyewe siye aliyepanda kwenye meli.

Sasa wakati mwengine tunakuwa sisi tuna haraka, lakini sisi tumesema kwamba kitambulisho chako cha Mzanzibari kinatufaa, barua ya sheha inatufaa, kitambulisho chako cha kazini kinatufaa, kitambulisho chako chochote ambacho kitakusema wewe kwamba ndiye fulani kinatufaa, alimradi uweze kusafiri ukijulikana ukitokezewa na tatizo uweze kujulikana ni nani, sasa hili jamani lina ubaya gani kwa ajili ya maslahi ya faida ya wananchi wetu.

Tunapambana sana na wenye vyombo kwa sababu wakati mwengine mwenye chombo huyu anafanya yule mwengine hafanyi, sasa abiria ukimwambia njoo huku kwangu sina haja ya kitambulisho anakwenda mbio. Tumejaribu kuweka na faini hapo ili kuweka hii hali itulie na bahati nzuri nitazungumza huko mbele, lakini Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi tumewashirikisha na sivyo kama anavyofikiria Mhe. Abass Juma Muhunzi kwamba hatujaishirikisha kamati hii. Tumeshazungumza nao na wenye meli na kamati hii ipo, wameshakwenda kuikagua meli ya Serengeti inakwenda Pemba ikahesabu abiria mmoja mmoja tuliwaambia twendeni leo mkahesabu abiria, wenye chombo hawakuambiwa na wakenda bandarini wakahesabu abiria wakakuta abiria hawakuzidi ile idadi ambayo wamepangiwa.

Tatizo walilolikuta ni kwamba kwa bahati mbaya sana meli za Pemba abiria 800, lakini watakwambia 1300 kwa sababu mtu ana watoto wanne hataki kuwakatia tiketi. Hilo ni tatizo jengine ambalo linatukabili nalo pia tunahisi tulifanyie kazi.

Mhe. Hamad Masoud Hamad, ansaema meli zote zina mapungufu. Inawezekana kweli, lakini si asilimia mia moja. Hapa Zanzibar watu wenye kununua gari mpya ni kidogo sana, lakini hata wawekezaji wa meli ni kidogo sana ambao wanaleta meli mpya. Kwa historia tumshukuru Mwenyezi Mungu hapa tulipofikia, miaka ya 1980 usafiri mzuri ulikuwa ni Ras Nungwi kwenda Dar es Salaam na sehemu nyengine, lakini sasa hivi wanajitahidi kidogo tuna meli za kileo kabisa za kina Bakhresa na wengine.

Kwa hivyo, tunawashukuru na tuwaunge mkono kwa sababu wakati mwengine wanasema sisi kuwekeza hapa Zanzibar hatupati faida, mtu pengine anatumia shilingi bilioni tano anakuja kupata faida ya shilingi milioni tatu au nne. Kwa hivyo, anafanya biashara upande mmoja anahudumia ndugu zake, lakini ukitaka biashara ya faida kubwa katika boti huwezi kuipata ndio maana wengi hawaleti boti ambazo ziko mpya.

Halafu alisema kwa nini mimi napendekeza ashtakiwe badala ya kusema tutamshitaki. Sheria inatueleza hivyo kwamba baada ya ajali ile na baada ya ripoti ndipo wizara kwa kupitia Mrajis wa Meli, tunaweza kufungua shtaka kwa huyo nahodha. Kwa hivyo, tutamshitaki kama ambavyo tumesema.

Kuhusu usalama wa boti, sisi tunazikagua boti kila muda tuliojipangia na baada ya ajali tumeongeza zaidi muda wa ukaguzi wa meli. Hatukagui sisi kama wizara kwamba tunapendelea, sisi tuna mkaguzi ambaye anafanya kazi hii na analipwa malipo kwa ukaguzi. Kwa hivyo, sisi tupo katika kulinda usalama wa wananchi wetu.

Kuhusu kujengwa meli, ndio yale niliyozungumza mwanzo kwamba imejengwa imeongezwa, lakini nafikiri mmeiyona ripoti yangu kwamba kuanzia sasa meli yoyote kabla ya kuongezwa huko inakonunuliwa itabidi mwenye meli aruhusu achukue kwa gharama zake, mkaguzi akaikague huko au mkaguzi ambaye tunamtambua sisi duniani aikague tupate *certificate* zake ndipo hapa tuwape usajili wa muda kabla kuileta meli yake, yaani ikakaguliwe kabla ya kufika Zanzibar huko huko iliko inakotengenezwa.

Tumeongeza kwamba sasa badala ya kuwa Mrajis tu anayetoa idhini, basi Waziri anayehusika na usafiri huu ndiye atayeidhinisha kwamba sawa nimeridhika sasa hiyo meli isajiliwe ili iweze kuja kufanya kazi zake.

Mhe. Zakiya Omar Juma, alisema ripoti imechelewa, nimeshazungumza. Pia, alisema kwa nini ripoti haikutaja *red cross*. Nafikiri tusingelitaja mmoja mmoja kwa sababu na watu wa Idara ya Maafa wangelisema na wao. Lakini ripoti imesema wale waliowataja halafu ikasema taasisi za serikali na za watu binafsi, sasa utaona na *red cross* inaingia hapo hapo, ukishasema na watu binafsi, taasisi za serikali basi na *red cross* wameingia hapo.

Kuhusu bodi kwamba ni kubwa, bodi haikuwa kubwa, bodi ilikuwa ni ya wataalamu na iliongozwa na mtu muadilifu Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar. Kwa hivyo, ripoti nafikiri haikuwa kubwa.

Kuhusu majeruhi wa ajali kusema maneno mengi, popote inapotokezea ajali inakuwa maneno mengi, kwa sababu hata hapa tulikuwa tunasikia, wengine wanasema kuna watu ndani ya meli tunasikia wanapiga simu huko chini kwamba njooni mnitoe mimi niko hai. Lakini ukweli hawakuwepo watu hao. Kwa hivyo, maneno ya mitaani yalikuwa mengi, lakini kila aliyekuwa na maneno kwa sababu hii rikodi ilifanyiwa kazi kwa uwazi na hakuna mtu ambaye alitishwa. Kwa hivyo, kila mmoja alikuwa ana haki ya kwenda kwenye bodi na kusema kwamba tatizo hili na hili na wengi tunawashukuru waliyotoa ripoti, watu 35 sio kidogo waliyokwenda kutoa ripoti hii.

Ni kweli kuna tafauti ya abiria na mizigo ambayo imeelezwa na hali halisi. Lakini ndio yale tuliyosema katika ripoti yetu kwamba kuna udhaifu katika wasimamizi wetu wa bandari Dar es Salaam. Sisemi bahati nzuri kwamba imetokea ajali, lakini haikutokea kwamba meli hii inatokea Zanzibar, kama Unguja au Pemba, imetokezea inatokea Dar es Salaam. Hata ile Meli ya Amana ya Pemba imetokezea inatokea Tanga.

Kwa hivyo, inawezekana na kwetu kuna udhaifu, lakini pengine kwa wenzetu umezidi zaidi katika usimamizi huo na pengine wenzetu wana mambo mengi

makubwa na nchi yao ni kubwa zaidi. Kwa hivyo, kuweka ile akili yao yote katika usimamizi huu kidogo kwao ni tatizo kubwa.

Kuhusu hatua za watendaji wa bandari ya Dar es Salaam, hili haliko katika mamlaka yangu. Lakini tumeshazungumza na Mhe. Waziri tulipokutana Pemba kwamba taasisi zetu za usimamizi za SUMATRA na Msajili wa Meli wawe na vikao vya mara kwa mara vya kubadilishana mawazo na mbinu za kuzuia matukio kama haya ambayo yanasababisha ajali.

Utaratibu wa fidia nimeshauzungumza, wale ambao wanastahiki watalipwa na mwenye chombo. Lakini kama nilivyosema mwenyewe kwa vyovyote na yeye ana bima sasa huwezi tu ukasema mimi Zakiya nilikuwa kwenye boti yako, lazima umpe vithibitisho ambavyo vitathibitisha aridhike kwamba wewe kweli ulikuwa katika boti yake, kama uliingizwa tu na nahodha wake mwenye chommbo, hajui basi hapo utakuwa umecheza mchezo wa pata potea. Kwa hivyo, hili nalo ndilo lile tunalolisisitiza kila wakati kwamba wananchi tujitahidi kufuata sheria.

Halafu aliunga mkono tu kwamba wananchi wawe makini na mimi nakushukuru. Hili nafikiri nikushukuru sana, umekuwa unalipigia kelele kwenye kamati kwamba wananchi wawe makini sana na kuona kwamba maisha yao yanakuwa salama kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman,yeye aliuliza nani anahusika kama meli inazama wakati imeshafunga gati? Meli hii imezama haijafunga gati, imezama inataka kufunga gati, kamba ya mwanzo ya kurushwa haikuwahi kufungwa imepinduka. Kwa hivyo, bado ilikuwa chini ya dhamana ya nahodha wa meli hii. Haikuwa ndani ya Mamlaka ya Shirika la Bandari au taasisi nyengine, hii ilikuwa bado haijafungwa, kama ilikuwa imefungwa, abiria wameshuka nahodha katoka halafu ikapinduka, pale yangekuwa mengine, lakini hii bado ilikuwa haijafunga gati inataka kufunga gati.

Halafu kitabu kuandikwa kwa Kifaransa. Halikuwa tatizo kwa sababu walishapewa kazi wenye meli waipeleke kwa wataalamu wa lugha hii wakakitafsiri, lakini ndio hayo makosa ya kiuzembe ambayo yamefanyika kuwa hakikutafsiriwa kitabu chenyewe kimezama na meli yenyewe imekwendanayo.

Kuhusu tiketi kwa vitambulisho kwamba tulifanya utafiti au vipi. Tulijitahidi sana kuangalia taratibu hizi na mimi kama Waziri ninayehusika na mambo haya bado nahisi kwamba kuna umuhimu wa kuendelea nayo. Tusiache kiholela hata kama ikiwezekana kwenye magari Zanzibar tungelikuwa tuna

tiketi basi ni vyema kuliko kuachia mambo yakenda kiholela. Kwa sababu wanaoumia ni wananchi wetu, wanaopata tabu ni wananchi wetu na watakaoteseka ni wao.

Hatua zilizochukuliwa tangu ripoti hii, kama nilivyozungumza katika ripoti yangu nimeanza kurekebisha baadhi ya mambo, kuna sheria zilikuwa hazijamalizika kutungwa pale kamati yetu tulipoiunda wizarani, tumefuatilia kwa karibu na karibuni zitamalizika. Lakini pia, ukaguzi tumeimarisha zaidi na uuzaji wa tiketi kwa vitambulisho umeanza. Kwa hivyo, hizo ni hatua za mwanzo ambazo zimeanza.

Pia, alisema kwa nini serikali ina kigugumizi kupeleka suala hili Mahakamani? Serikali haina kigugumizi, lakini kama nilivyosema huwezi kupeleka kesi Mahakamani wakati ripoti hujaitoa. Kwa hivyo, kuanzia sasa nafikiri nyinyi wenyewe mtashuhudia kwamba hatuna ya kigugumizi cha kupeleka kesi hii Mahakamani.

Mhe.Abubakar Khamis Bakary, alisema ripoti ya kamati ya bodi na Waziri inatofautiana. Hilo ndio lazima iwe hivyo, kwa sabbau wao wameniandikia mimi na mimi ndiye ninayetakiwa nitoe ripoti halisi ya serikali kwa jinsi mambo yalivyo, lazima kuna mambo mnakubaliana na mengine unachambua ya kisheria pengine wao sheria nyengine zimewapita.Hivyo, unaangalia tunaona kwamba lazima zitofautiane.

Jengine, kubadilishwa kwa meli kutoka mizigo mpaka abiria, nimeshalizungumza kwamba sheria inaruhusu kuwa *land craft* ya mizigo na abiria alimradi ufuate sheria. Kwa hivyo, hili linaruhusiwa.

Halafu kwa nini bima walikubali kuiwekea bima meli hii? Ukataji wa bima hauhusiani na wizara yangu mimi. Sisi mwenye chombo tunampa leseni baada ya kutuhakikishia kwamba ana bima na mambo yote yanayostahiki. Kwa hivyo, Shirika la Bima na mwenye meli lazima walikuwa na mazungumzo yao na wamekubaliana wenyewe, hata kulipana sisi hatuulizi mmeshamlipa au bado, hiyo si kazi yetu wakimlipa sawa, wasipomlipa watajuana wenyewe, lakini sisi hatuhusiki na bima.

Vile vile, aliuliza kwamba hizi meli zinachukua abiria wangapi na akatolea mfano wa Meli ya Serengeti, akasema mbona inachukua watu wengi. Uwezo wa Meli ya Serengeti kuchukua abiria ni 1000, lakini siku hizi mimi kwa ile tahadhari ambazo Waheshimiwa wananipa sana huwa nawaambia wakaguzi wangu hebu nendeni mkaikague, mbona kila siku nasikia hivi, wanakwenda wanakuta salama, tena wananambia mkuku wake mzuri zaidi kuliko meli nyengine, kila wakienda wananambia vile vile. Nikawaambia pamoja na hayo

pakieni watu 850 msizidi hapo yaani nashusha mimi kila wakati, wakati mwengine wananambia tuwape watu 900 nawambia wapeni 850. Lakini bado meli ile uwezo wake ni watu 1000.

Lakini tatizo ni kama nilivyosema Serengeti ndio meli ya ukombozi kwa Pemba sasa hivi, ikienda na watu 800 watu wenyewe wana lishe nzuri wana watoto 400 au 500, sasa tukisema pale bandarini tunawarejesha wale watoto kishindo, wengine basi, wanachukua ndizi, kuku, mabungo na kadhalika na wakati mengine tatizo ambalo lipo na tunajitahidi hili tuliweke sawa kwamba angalau basi ile mizigo ikae sehemu moja sio mzigo na mtu hapo hapo, mtu anataka kukaa na kuku wake hapo hapo hamuamini mwenzake.

Kwa kweli kama itakuwa hivyo, meli ukaingiza kuku na vitu vyengine bila shaka ukifika Zanzibar utasema meli ile inanuka, lakini wanaachia wanafanya mambo yote lakini kwa taratibu hizi tofauti na ukipanda boti ya Bakhresa ile ya *speed* huwezi kukuta mambo kama hayo, kwa sababu mle mtu haingii na kuku wala mgomba wake, mle dakika 45 uko Dar es Salaam kimya.

Kwa hviyo, nafikiri tukubaliane, unajua haya mambo tukisema tunaifungia moja kwa moja ile hatari yake ni kubwa zaidi, lakini ikiwa ina kasoro tutaizuia, hatuwezi kwa sababu inatakiwa iende Pemba tukasema tena tusiizuie kwa sababu inakwenda Pemba, ikiwa na kasoro nayo wakaguzi wetu wakisema mimi nitasema hii isiende izuiliwe mpaka ifanyiwe marekebisho na kwa sababu hatujaweka muda kwamba ikifika miaka 50 ikaguliwe basi tutaendelea mpaka tutakapoona kwamba sasa mwenyewe imemshinda.

Halafu Mhe. Salmin Awadh Salmin, kwamba taarifa imechelewa nimeshajibu, waliopoteza mali zao hawajalipwa fidia, ndio ripoti hii inaagiza sasa, muda gani wa kulipwa fidia, ndio kwanza unaaza kwa sababu ripoti ilikuwa haijasema lolote, ndio kwanza tumeisoma na kuileta hapa.

Pia, alisema mmiliki wa meli akishindwa kulipa atachukuliwa hatua gani? Kwa wale ambao sheria inawaruhusu wana vielelezo vyote wakishindwa kulipwa kwanza, hatua ya mwanzo wanakuja kwa Mrajis wa Meli wataleta malalamiko yao, tutawachukulia hatua, tukishindwa taratibu za kimahakama zitafuata.

Halafu aliuliza kiasi gani cha fedha kilichotumiwa na bodi? Bodi hii ilitumia zaidi ya shilingi milioni ishirini na sita, karibu milioni ishirini na nane nafikiri.

Mhe. Said Ali Mbarouk, aliuliza kwa nini mkaguzi wa meli asishtakiwe? Tumeeleza katika ripoti ile, mkaguzi kaikagua meli hii, lakini tunaona kasoro yake ilikuwa kwenye *bottom plate*, hakwenda tunavyohisi sisi kwa sababu ndiko kwenye matatizo. Kwa hivyo, hatua ya mwanzo huwezi kumpeleka

Mahakamani kwa suala hilo na imefanya kazi sana na nini tukaona kwamba huyu atatoleshwa faini kwa mujibu wa sheria zinavyoturuhusu.

Pia, aliuliza chombo gani kinachomchagua Mrajis. Mrajis anachaguliwa na Waziri na wafanyakazi lini watapewa mafunzo.Tunaendelea na mafunzo na Mhe. Said anawajua baadhi ya wafanyakazi wetu ambao wamepewa mafunzo wa muda mrefu na sasa hivi ni wataalamu. Kwa hivyo, nafikiri alikuwa ananipa changamoto niendelee tu kuwapa mafunzo, lakini anawajua.

Afisa Mrajis tunaimarisha ilivyokuwa mwaka juzi sivyo ilivyo leo, walikuwa wakitumia katika jengo letu la wizara, walikuwa na chumba kimoja wafanyakazi 7. Sasa tumewaimarisha, tumewapa jengo wanafanyakazi vizuri na kama nilivyosema Mwenyezi Mungu akipenda tunatarajia kuanzisha mamlaka rasmi ambayo imeshapitishwa na Baraza hili ya usafiri baharini. Kwa hivyo, tutajiimarisha zaidi kwa hatua hiyo.

Halafu alisema meli zinazokwenda Pemba ni chakavu, serikali inachukuwa hatua gani? Hatua ambayo tunachukuwa hivi sasa ni kuhakikisha kwamba meli ziko katika usalama, zenye uchakavu hatuwezi kuzifanya ziwe mpya, lakini tunahakikishia hizo hizo chakavu zinakuwa salama hazihatarishi maisha ya wananchi wetu kwa wakati wowote wa safari.

Mhe. Abass Juma Muhunzi, anasema kuna taarifa kuwa nahodha hakuruhusiwa kwenda kwenye mchanga. Mhe. Spika, kwa kupitia Baraza lako hili tukufu, naomba niseme kwamba si kweli watu wote wakiwemo wenye Boti za *Flying Hourse* na wengine wanathibitisha kwamba huyu hakuwa na mawasiliano yoyote, alifanya kuweka meli kwenye mchanga na nahodha wa *Flying Hourse* alimuuliza mbona meli yako inakwenda upande upande, lakini yeye hakujibu vizuri na kuendelea na safari yake. Kwa hivyo, hiyo ya kwamba alikatazwa sijui hakuna suala hilo. Yeye mwenyewe tu alipima labda akaona atafika salama na akaona labda kuingia kwenye mchanga ni gharama.

Mhe. Spika, ukweli kapteni huyu pia anabahati mbaya kibinadamu. Ilivyozama Meli ya Amana Pemba kapteni alikuwa abiria wa kawaida, lakini akasalimika. Kwa hivyo, meli hii yeye alikuwa kapteni, sasa kabla ya hatua hizi tumeshamzuilia leseni yake tangu wakati ule wa ajali. Kwa sababu tumeona aa. Kwa hivyo, Kapteni huyu ana mkosi, kwa hivyo, kidogo atulize akili yake. Tukimpeleka Mahakamani ndio huko tutamuuwa, lakini sasa hivi tumemzuia huyu moja kwa moja, hata hawa mabaharia nao pia tumewazuia sasa hivi. Kwa hivyo, tulichukua hatua za dharura katika kuliweka sawa jambo hili.

Mhe. Spika, matatizo yaliyosababisha kuzama haraka. Nafikiri umeona ile ripoti mambo mawili makubwa kwamba maji yalikuwa yakiingia kwa kasi na

*bottom plate* kule chini mbovu.Kwa hivyo, imeingia maji haraka na ikazama kwa haraka. Kwa hivyo, zile taarifa ndio zilizosababisha izame kwa haraka.

Halafu alizungumzia kwa nini zinaruhusiwa kuingia meli bila ya kuweka muda kwa meli hizo, yaani uundwaji wake. Nimelisema hili kwamba bado hata hizi sheria za kimataifa hazisemi kwamba meli ziwe na miaka mingapi. Isipokuwa sisi tutaangalia kama sheria inawezekana kweli kufanya hivyo, lazima tutatazama na utafiti kwa kwengine kama iko tutafanya hivyo. Je, tunaweza tukaweka miaka 10, 20, 30 au 50. Je, tukiweka hizo sheria wananchi wenyewe na wawekezaji wenyewe wataweza kuleta meli na kutoa huduma kwa wananchi. Hilo tutaliangalia kwa kina.

Mhe. Spika, nani ana kosa kwa kutokupelekwa meli chelezoni. Mwenye kosa anakuwa mwenye meli kwa sababu sisi sheria yetu inasema wapeleke chelezoni. Tunajitahidi sana meli zetu hizi kuzilazimisha na wakati mwengine ikichelewa kuzipiga faini. Wanajitahidi kwenda, nafikiri *Sea Express* sasa hivi iko Mombasa chelezoni.

Mhe. Spika, wakati mwengine unaweza ukenda chelezoni na tatizo moja, ukarudi huku kuna tatizo jengine limetokezea. Lakini tunajitahidi sana kuhimiza kwamba meli ziende chelezoni kwa wakati ili kuweka maisha bora kwa wananchi wetu.

Halafu alizungumzia tumejiandaa vipi baada ya tukio lile na akatolea mfano Serengeti inajaza sana. Nimeshazungumza Serengeti na meli zote tunazikagua tena, tumeanza ukaguzi mpya baada ya tukio lile. Nafikiri Serengeti tumeshaikagua kama mara mbili au tatu, kabla ya wakati wake tumeikagua, tumefanya ukaguzi wa kushtukiza na ukaguzi wa kawaida, lakini bado tumeona hilo linalozungumzwa halijawa la ukweli sana.

Kuhusu migongano baina ya wizara na wenye meli na akapendekeza kwamba Kamati ya Mawasiliano iingilie kati. Waheshimiwa Wajumbe Kamati ya Mawasiliano tumeshawaita, tulikutana na wenye meli wakasema yao wala hatukuwaambia wazibe mdomo. Tatizo ni vigumu kwamba kila baada ya miezi miwili au mitatu uwaite wenye meli na kamati. Kwa sababu na wenye meli nao wanalalamika wanasema kila siku kamati inatuita, sasa sisi tuna mambo mengi.

Kwa hivyo, tumeangalia labda miezi sita tuwe tunafanya kikao mara moja na wenye meli na Kamati yetu ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi. Hilo linawezekana na linaweza likaleta tija kwa pande zote.

Mhe. Spika, tunapokutana nao wenye meli, wanapata fursa ya kusema yao na kamati nayo inatusaidia sisi wizara. Kwa sababu tunapozungumzia wananchi

wa Pemba nikizungumza mimi peke yangu, naonekana pengine sifanyi haki, lakini na kamati nayo ikisema vile vile ninavyozungumza mimi kidogo inaleta uzito na nguvu zaidi.

Mhe. Mohamed Ali Salim, alizungumza kwanza hatua gani zinachukuliwa kuepusha ajali za angani. Bahati nzuri kuna Mamlaka ya Usafiri na Usalama wa Anga, hii na sisi tumo tunatoa mawazo yetu, tunashauri vizuri. Katika hayo mambo ya kusababisha kwamba ajali za angani zisiwe nyingi tumejiimarisha katika viwanja vyetu vya ndege na sasa hivi *runway* iko nzuri tunaendelea kuijenga. Mimi jana nilikuwepo mpaka saa nne za usiku nimeangalia kazi inakwenda vizuri. Lakini pia, vifaa vinaendelea kutafutwa vya kuimarisha uwanja wetu wa ndege kupunguza hizo ajali. Kwa hivyo, hili nalo ni jambo jema la kufanya kwamba tupunguze ajali.

Baada ya ajali hii, hatua gani nyengine zinachukuliwa. Nafikiri nimeshasema tunachukua hatua si kwa kumkomoa mtu, tunachukua hatua kwa kujiepusha na madhara. Kwa hivyo, ni jambo jema kwamba sote tushirikiane hili jambo liwe sawa.

Sababu gani zilizosababisha nahodha akatae kupeleka meli mchangani. Hata mimi zisijui, hata bodi haikusema sababu gani. Lakini hakupeleka. Kwa hiyo, maadam hakupeleka na imezama meli ndio tunamchukulia hatua, pengine mwenyewe atasema Mahakamani sababu gani zilizosababisha asiende. Atakuwa na mashahidi wake na sisi tuna mashahidi wetu. Kwa hivyo, itaonekana je, ni kweli kama kasema au hakusema itakuwa huko.

Meli iliyokuwa haitumiki inapelekwa wapi. Unaruhusiwa mwenyewe kukata *scraper* na mambo mengine yoyote yale unayoweza, maadam ni meli yako, lakini nina hakika huirejeshi Ulaya vile ilivyokuja. Pengine yapo bado pale tunafanya bidii waje wachukue wenyewe, lakini kidogo wagumu na tukiwapiga faini wanakuja kwa Waheshimiwa wanalalamika kwamba tunaumizwa vibaya, lakini jitihada zinaendelea.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman, aliuliza kwa nini hakuna nyaraka za meli. Mhe. Spika, nyaraka zipo, baadhi ya nyaraka ndio zilikuwa hazikuonekana zimezama na meli.

Halafu mwaka wa kuundwa meli umefichwa, hatua gani zimechukuliwa. Kwa sababu mwaka bado ilikuwa si kitu cha msingi sana katika uletaji wa meli hapa, labda huko katika mambo ya bima. Lakini kwetu sisi hakina msingi sana, meli ikikaguliwa ikionekana inakidhi viwango tunairuhusu meli kuja bila ya tatizo lolote. Sasa kama kaunda mwaka 1964, 1965, 1975 ilikuwa hakuna sheria

ambayo inakataza meli hii kuingia Zanzibar, alimradi ikifika hapa ikaguliwe iweze kutoa huduma kwa wananchi.

Halafu aliuliza pia, meli zilizokuwepo sasa hivi zinakaguliwa kila mwaka. Ni kweli meli zote zinakaguliwa kila mwaka, hakuna meli ambayo haikaguliwi kila mwaka hapa Zanzibar.

Halafu kasema dereva akipata ajali anakamatwa. Huyu alikamatwa, akapelekwa polisi nae, akachukuliwa maelezo halafu akaachiwa kwa dhamana, lakini sasa kesi ndio itafunguliwa. Kwa hivyo, taratibu zitaendelea.

Halafu aliuliza, je, meli mbovu zinaweza kufutiwa leseni. Ndio, meli yoyote ile ambayo ni mbovu haifanyi kazi zake vizuri, inakiuka taratibu, haiwalipi mabaharia wake, haifuati taratibu za bandari, hata kama nzima tunaweza tukaifutia leseni au kuisimamisha. Tunaweza kuzungumza nao, tukawapiga faini, tukawafutia leseni yao.

Mhe. Spika, Mhe. Juma Duni Haji, aliuliza hatua zinachukuliwa, nidhamu inachukuliwa, lakini wizarani kweupe hakuna yeyote. Mhe. Spika, hawa wengine walioambiwa watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria za kazi ni watu wa wizara. Lakini huwezi pale wizarani ukamchukulia mtu hatua kwa sababu meli imezama na yeye yuko Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, wala hahusiki na kosa lolote lile. Itakuwa sio kwamba tunamchukulia hatua, itakuwa tunamuadhibu bila ya makosa. Kwa hivyo, wale ambao wanahusika tunatazama sheria zetu za kazi zinaturuhusu vipi.

Halafu Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim, kiasi gani cha gharama kilichotumika katika uokozi. Gharama zote zinazidi shilingi milioni 200 na karibu hizi zote wamelipa Shirika la Bandari. Inatakiwa sasa mmiliki wa meli azilipe yeye kurejesha Shirika la Bandari. Bado meli yake hajaichukua, kuna mgogoro, nae kapinga sijui kama atakwenda Mahakamani au vipi, lakini anatakiwa azilipe yeye. Sio meli kuiopoa tu pale, hata meli kwa mujibu wa sheria ukiwa na tatizo baharini ili uje uokolewe, lazima kwanza uulizwe, utanilipa au hunilipi.

Wakati mwengine mimi juzi niliposikia Sea Gull imepata matatizo nikampigia Mkurugenzi wa Shirika la Bandari, akaniuliza watatulipa? Nikamwambia sijui vipi, lakini ikibidi sana mimi kama Waziri naagiza wende tu ukaliburure halafu baadae tutajuana huku huku tutaizuia au vipi, lakini kwanza maisha ya watu mbele. Bahati nzuri ikaweza kufika salama.

Kwa hivyo, sheria zinasema hivyo kwamba katika uokozi wa baharini lazima kwanza umlipe kwa sababu pengine mtu anatumia gharama kubwa sana.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuishukuru sana Wizara ya Miundombinu na Mhe. Waziri, kwambwa kwa kutusaidia kutuletea lile ndovu. Hata hizi gharama nyengine za ndovu humu hatujaingiza. Kwa hivyo, tunashukuru sana kwamba walitusaidia sana katika kipindi kigumu, nafikiri haya ndio mashirikiano mazuri.

Mhe. Spika, nafikiri Mhe. Burhan Saadat Haji, alikuwa mtu wa 16 yeye alisema tuunde kitengo. Mhe. Spika, vitengo vipo labda tuviimarishe. Sawa hilo tunakubali kwamba vipo tutaviimarisha chini ya Mamlaka ya Usafiri wa Baharini.

Pia, Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis, aliuliza kwa nini hatuna *traffic* wa baharini. Sasa sijui vituo vyao viwe juu au wajengewe baharini hivyo vituo vya *traffic*. Mhe. Spika, hili linataka mjadala kidogo, nitakaa mimi na wataalamu wangu tuangalie tunawashirikisha vipi polisi katika safari hizi.

Kwa sababu kulikuwa pia kuna wazo ambalo sio baya, sijui kama tutaliweza kwa gharama. Hizi boti pamoja na kwamba nzima zikienda Dar es Salaam kuwe na askari angalau mmoja wawili na zikirudi ili kupunguza uharamia ndani ya boti zenyewe. Kwa sababu wakati mwengine boti zinakuwa nzima, lakini kuna vitendo vinafanyika ndani ya boti si vya kibinadamu. Kuna kipindi kuna abiria mmoja alimchoma mwenzake kisu, kuna mwengine anamuibia mizigo mwenzake.Kwa hivyo, nafikiri hili jambo linazungumzika na tunaweza tukalifanyia kazi vizuri.

Halafu, alisema sio kweli kwamba kila mpiga mbizi ni muokozi. Sawa lakini wakati wa shida kila ambaye anajua kupiga mbizi tulimuhitaji atusaidie na wengine waliweza kufanya kazi vizuri, wengine kama ulivyosema wewe mwenyewe walikuwa wapiga mbizi tu, lakini hawakutusaidia sana. Sasa mafunzo ni muhimu.

Mhe. Spika, haya mambo mengi yaliyozungumzwa kuanzia bodi yenyewe mpaka Waziri mwenyewe yanahitaji pamoja na dhamira na nia, lakini pia yanahitaji na uwezo wa serikali ukiwa mkubwa.

Katika moja ya taasisi ambazo vifaa vyake ni ghali sana ni wizara yetu ambapo karibu vifaa vyake vyote ni vya kiufundi. Kama alivyosema Mhe. Hamad Masoud Hamad, sisi nafikiri na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ni wizara za kiufundi sana.

Mhe. Spika, sisi huwa hatununui kifaa cha shilingi milioni 6 au 7, havipo duniani vifaa vya aina hiyo. Kwa mfano ukisema mnyororo wa *bulldozer* basi shilingi milioni 50 uwe nazo kwendea juu. Sasa na huku ukija kwenye

ma-*crane* na mengineyo shilingi bilioni 2 kwendea mbele, ndio pesa ndogo ya kuizungumza. Kwa hivyo, pamoja na dhamira nzuri ya kuwa na vifaa vya kiuokozi, lakini la mwisho lazima tuwe na fedha za kufanyia shughuli hizo.

Lakini kwa uwezo wetu tulionao tutajiimarisha, tumejiimarisha bandarini ,sasa hivi sivyo tulivyokuwa na tunaendelea kujiimarisha. Wiki mbili zilizopita tuliwaita Makamanda wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi tukazungumzia namna bora ya kuimarisha huduma za Zimamoto bandarini na wamesema mahitaji yao. Lakini mimi nikamuagiza Mkurugenzi wa Shirika la Bandari akae nao wapange mipango mizuri ili kuwasaidia Zimamoto kuweza kutusaidia pale bandarini. Ingawa mambo haya ya uokozi bandarini Zimamoto wanahitajika, lakini na taasisi zetu nyengine ziimarike kwa sababu sio kila jambo kwamba litakuwa la moto, kuna ajali nyengine ambazo Zimamoto hawatoweza kutusaidia.

Ilipotokezea ajali ya kuungua kwa MV Aziza I na Aziza II kule Mtoni, kikosi hichi kilitusaidia sana kupita kiasi. Kwa hivyo, napenda niwashukuru sana kwa juhudi zao walizozifanya.

Mhe. Spika, mwisho niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwamba wakati wa kadhia ile kila mmoja alitaka kutoa msaada wake. Wengine nilikuwa nawahurumia pengine watapiga mbizi halafu wasije tena juu. Kwa hivyo, kina Mhe. Zakiya Omar Juma, nilikuwa nawahofia sana kwamba asije akaona kwamba aende chini akatafute mtu na baadae yeye asirudi tena. Mhe. Spika, tunawashukuru wote na nakushukuru tena wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha ripoti leo hii.

**Mhe. Spika:** Nakushukuru sana Mhe.Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi. Sasa Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri anataka akaifanyie kazi ripoti hii. Tuone basi wale wanaoipokea na kuikubali ripoti hii wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. Ripoti iko tayari Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi kwa kufanyiwa kazi na wizara na hatua nyengine zote.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe shughuli zetu kwa leo naona kama zimekwisha na kwa sababu hiyo itakuwa hakuna sababu ya kuja jioni.

## KUAHIRISHWA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwa kuwa shughuli zilizopangwa kwa ajili ya kikao cha leo zimemalizika kabla ya wakati wake, naomba kutoa hoja Baraza liahirishwe mpaka kesho saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana kwa mashirikiano makubwa ya kufanya kazi. Kazi yetu ya kesho ni moja, hoja iliyowasilishwa kwa Katibu na ikafika kwangu, iliyoelekeza kutoa taarifa kwa Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwamba hoja hiyo iwasilishwe kesho, wakati huo shughuli zote zile za serikali zitakuwa zimemalizika.

Kwa hiyo, naomba sasa niahirishe kikao hichi mpaka kesho tarehe 28 Januari, 2010 saa 3:00 barabara za asubuhi ambapo tunategemea hoja ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary itawasilishwa na yeye hiyo kesho Mwenyezi Mungu akipenda. Ahsanteni sana.

*(Saa 7.00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 28/01/2010*
*Saa 3.00 asubuhi)*